

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji.

Usimamizi wa Mazingira na Uhifadhi wa Viumbe hai Anuai kwenye Mimitu, Maeneo ya Miti, na Ardhi Owevu ya Delta na Uwanda wa Mafuriko wa Rufiji¹.

Kuchanganya Maarifa Ya Kimila Na Ya Kisayansi Kwa Mwamko Wa Mazingira

**Maadhimisho Ya Siku Ya Maeneo Ya Ardhi Owevu Duniani Iliyofanyika Utete, Rufiji
Tarehe 2 Februari, 2003**

Doody K.Z., John, P, Mhina, F. na Hamerlynck O.



Ripoti ya Utaalamu Na. 41

Machi 2003

Kwa taarifa zaidi wasiliana na

Meneja mradi,

Mradi wa usimamizi wa mazingira Rufiji

S.L.P 13513

Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: 023 2402519/20 utete Rufiji au 0741 322366 Dar es Salaam

Barua pepe: rempute1@bushmail.net or iucndar@epig.or.tz

¹ Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inatekeleza mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji pamoja na msaada wa kitaalamu toka IUCN – Umoja wa Hifadhi Duniani, na kugharamiwa na Ubalozzi wa Kifalme wa Uholanzi.

Rufiji Environment Management Project – REMP

Project Goal: To promote the long-term conservation through ‘wise use’ of the lower Rufiji forests, woodlands and wetlands, such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area’s inhabitants are secured and enhanced.

Objectives

- To promote the integration of environmental conservation and sustainable development through environmental planning within the Rufiji Delta and Floodplain.
- To promote the sustainable use of natural resources and enhance the livelihoods of local communities by implementing sustainable pilot development activities based on wise use principles.
- To promote awareness of the values of forests, woodlands and wetlands and the importance of wise use at village, district, regional and central government levels, and to influence national policies on natural resource management.

Project Area

The project area is within Rufiji District in the ecosystems affected by the flooding of the river (floodplain and delta), downstream of the Selous Game Reserve and also including several upland forests of special importance.

Project Implementation

The project is run from the district Headquarters in Utete by the Rufiji District Administration through a district Environmental Management Team coordinated by the District Executive Director. The Project Manager is employed by the project and two Technical Advisers are employed by IUCN.

Project partners, particularly NEMC, the Coast Region, RUBADA, The Royal Netherlands Embassy and the Ministry of Natural Resources and Tourism, collaborate formally through their participation in the Project Steering Committee and also informally.

Project Outputs

At the end of the first five –year phase (1998-2003) of the project the expected outputs are:
An Environmental Management Plan: an integrated plan for the management of the ecosystems (forests, woodlands and wetlands) and natural resources of the project area that has been tested and revised so that it can be assured of success - especially through development hand-in-hand with the District council and the people of Rufiji.

Village (or community) Natural Resource Management Plans: These will be produced in pilot villages to facilitate village planning for natural resource management. The project will support the implementation of these plans by researching the legislation, providing training and some support for zoning, mapping and gazettement of reserves.

Established Wise Use Activities: These will consist of the successful sustainable development activities that are being tried and tested with pilot village and communities and are shown to be sustainable

Key forests will be conserved: Forests in Rufiji District that have shown high levels of plant biodiversity, endemism or other valuable biodiversity characteristics will be conserved by gazettement, forest management for conservation, and /or awareness-raising with their traditional owners.

Yaliyomo

1	Utangulizi	1
1.1	Kamati ya Mipango	1
1.2	Wasaidizi.....	2
1.3	Kipindi cha mazoezii ya matembezi ya viumbe.....	3
1.4	Kikundi cha Tathmini	4
1.5	Shughuli za baada ya tukio	5
2	Tathmini ya Shughuli za Sherehe.....	6
2.1	Kupanga sherehe	6
2.2	Kuzitangaza sherehe.....	7
2.3	Matembezi ya Viumbe	7
2.4	Mchezo wa Kuvua Samaki.....	8
2.5	Jedwali la Ugunduzi.....	9
2.6	Mashindano ya uchoraji	10
2.7	Bango la ndege wa ardhi owevu	11
2.8	Kona ya kupaka rangi.....	11
2.9	Monyesho ya picha	12
2.10	Gandisha maziwa katika mchezo wa ramani	12
2.11	Mchezo wa Mzunguko wa Maji.....	13
2.12	Chemsha Bongo – Kutafuta maneno	13
2.13	Bango la Mimi ni Nani.....	14
2.14	Mchezo wa Mimi ni Nani	14
2.15	Mchezo wa Utando wa Maisha wa Ardhi owevu.....	14
2.16	Mchezo wa Kuigiza.....	15
2.17	Kwaya	16
2.18	Utoaji Zawadi.....	16
2.19	Uwasilishaji Wa Baiskeli Kwa Wakusanyaji Wa Data Za Maji	17
2.20	Chemsha Bongo	17
2.21	Video.....	18
2.22	Mahudhurio	18
2.23	Mpango wa Jumla wa Sherehe.....	18
2.24	Tathmini ya Washiriki.....	19
2.25	Mada nyingine Zilizoibuka wakati wa Majadiliano	19
3	Viambatisho	20
3.1	Kiambatisho cha 1: Taarifa	20
3.2	Kiambatisho cha 2: Maandishi ya Kiswahili na Kiingereza ya	21
3.3	Kiambatisho cha 3: Bango La Ndege.....	23
3.4	Kiambatisho cha 4: Ratiba	26
3.5	Kiambatisho cha 5: Jedwali la maneno	27
3.6	Kiambatisho cha 6: Mimi ni nani? Unaweza kubuni kilichofichwa.....	29
3.7	Kiambatisho cha 7: Maswali na majibu ya Chemsha Bongo	30
3.8	Kiambatisho cha 8: Taarifa ya tovuti Utete Inasherehekea Siku ya Ardhi owevu Duniani 32	
3.9	Kiambatisho cha 9: Orodha ya washiriki walioalikwa katika sherehe za Siku ya Ardhi owevu Duniani	35

Picha zote zimepigwa na Kathryn Doody, isipokuwa ukurasa wa 5, 10 juu, 5, 17 chini na 18 zimepigwa na Gratian Luhikula

1 Utangulizi

Ripoti hii ni muhtasari wa shughuli zilizofanyika kama sehemu ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira, Rufiji, katika kuadhimisha siku ya Ardhi Owevu Duniani huko Utete, tarehe 2 Februari, 2003 na tathmini ya shughuli.

Timu ya Usimamizi wa Mazingira ya Wilaya (TUM), chombo kinachounganisha wafanyakazi wataalamu wa idara kuu za serikali ya mitaa zinazohusikana na wawakilishi wa maliasili, ardhi, kilimo, elimu, maendeleo ya jamii, mipango, nk., toka wabia (miradi mingine ya mazingira wilayani), madiwani wa kuteuliwa wawili na wafanyakazi wa MUMARU. Hufanya mikutano yake ya kawaida kila Ijumaa ya kwanza ya mwezi huko Utete. Katikati ya mwezi Desemba, mwaka 2002, CTA ya REMP ilitoa taarifa kuhusu Thamani ya Ndege wa majini kimataifa na siku ya Ardhi Owevu Duniani kwa TUM, akiomba mawazo na mapendekezo jinsi Rufiji inavyoweza kushiriki katika sherehe hizi za kilimwengu (kiambatisho cha 1). TUM ya mwezi January iliamua kuwa sherehe zote mbili hizi zingeweza kufanyika siku moja na ikaunda kamati ya mipango, kushughulikia maandalizi.

1.1 Kamati ya Mipango

Sherehe zilipangwa na kutekelezwa na kamati ya mipango iliyochaguliwa na wajumbe wa Timu, ya usimamizi wa mazingira. Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango alikuwa Mheshimiwa Diwani Athumani K. Palla, katibu alikuwa Bw. Peter John (DALDO), wajumbe wa kamati walikuwa Mheshimiwa Diwani Mwajabu Kingwande, na Bw. John Eniyoye (DGO). Kwa nyongeza Dk. Oliver Hamerlynck (CTA ya MUMARU) na Bw. Frederick Mhina (MM wa MUMARU) alichangia katika mpango wa sherehe. Kamati ilikutana tarehe 13 Januari, 2003 kuunda ratiba ya kazi.

Kamati iliweka lengo lake kuwa:

Kujenga mwamko juu ya kazi za ardhi owevu, kwani ni muhimu kwa maisha katika Rufiji (na hivyo dhamana ya chakula), mila za ardhi owevu na dhima yao katika kuhifadhi Viumbe hai anuai.

Iliamuliwa kuwa mkazo uwe katika kuunganisha rasilimali mbalimbali: dhima ya mafuriko kwa kilimo, uvuvi, misitu, n.k. Ujumbe muhimu wa kutoa ulikuwa: hakuna budi kuzijali ardhi owevu zetu kwa kuwa zinatujali. Kwa upande wa utaratibu ilipendekezwa kuifanya sherehe iwe ya kushirikisha kiasi iwezekanavyo na kukwepa mihadhara mirefu na hotuba kubwa. Iliamuliwa kufanya kazi hasa kwa kupitia mawasiliano ya moja kwa moja kati ya washiriki mbalimbali na kikundi cha wahusika, kupitia mazungumzo, kutumia maswali na majibu na, mengi iwezekanavyo, mahali ambapo masuala ya ardhi owevu yangeweza kuchunguzwa moja kwa moja.

Ilielezwa wazi kuwa dhamira ilikuwa ni kuwa na shughuli yenye gharama ndogo – athari kubwa. Hivyo iliamuliwa kuweka kituo cha sherehe huko Utete na ardhi owevu zinazoizunguka. Hadhira lengwa ingekuwa viongozi na watoa maamuzi wa jamii, wajumbe wa TUM na walimu wa shule za Utete na wanafunzi wao. Kutngekuwa na sehemu kuu mbili za sherehe:

- Matembezi ya viumbe mapema asubuhi ambayo, kwa sababu za kiutendaji yangekuwa na idadi ya washiriki yenye mipaka, na
- Programu ya wazi ya mchana, ambayo watu wa kawaida/kwa ujumla pia watakaribishwa.

Kamati ya mipango iliandika rasimu ya ratiba ya kazi na bajeti na kazi zikagawanywa. Idara ya Elimu ya Wilaya ilizialika shule kushiriki katika mashindano ya kuchora ardhi owevu na ndege wa ardhi owevu kama mada yake. Michoro ilitakiwa iwe imefika ilipofika tarehe 30 Januari ili iweze

kupangiwa bajeti kabla ya sherehe na kazi zilizoshinda zionyeshwe. DALDO ilitayarisha muhtasari wa kazi za ardhi owevu katika lugha ya kiswahili na hii ilipelekwa mashuleni kama taarifa ya awali. Kikundi cha maigizo cha Utete kiliombwa kupanga mpangilio wa matukio kwa ajili ya onyesho linalohusiana na ardhi owevu. Waandalizi walifafanua kuwa mpangilio huo wa matukio usijifunge katika usimamizi endelevu wa kawaida na vikwazo vya uchekekeshaji bali ule utakaokwenda kwa undani kwa kutilia mkazo manufaa muhimu ya kiwango cha usimamizi kilichokubalika. Utaratibu wa ugavi na usafirishaji, vifaa kwa ajili ya matembezi ya viumbe na maonyesho, n.k. vinahitaji kupangwa. Ilikuwa mahali pa sherehe pawekwe kivuli. Taarifa muhimu za matukio zilijadiliwa. Wasaidizi toka idara ya elimu walihamasishwa na kushiriki mara chache katika mikutano ya kamati ya mipango. Vipindi vifupi vya taarifa ya utekezaji vilifanya tathmini ya maendeleo katikati ya matukio.

1.2 Wasaidizi

Kamati ya mipango iliamua aina ya wasaidizi wanaohitajika na kwa kushirikiana na wafanyakazi wa wilaya ili wateua wafutao kusaidia katika utayarishaji na utekelezaji wa sherehe:

1. Mwenyekiti wa Kamati ya Wilaya ya Huduma za Kiuchumi, Kazi na Mazingira, Mhe. Mgeni A. Monero.
2. Wasaidizi wenyeji wenye uzoefu na eneo owevu na ndege; Mzee Abdulrahman Mnyige, Mzee Habibi Omari, Mzee Mohamed Omari, Mzee Hemed Mshamu, Mzee Malik Athumani, Mzee Mkombya Matibwa, Mzee Masela Hamisi.
3. Msaidizi mwenyeji katika masuala ya maji, usomaji wa ubao wa hatua, umuhimu wa mafuriko na haja ya kukusanya na kuhifadhi taarifa za wenyeji za viwango vya maji: A. B. Mwakalinga, Afisa kilimo Wilaya.
4. Wasaidizi wenyeji katika uvuvi: Vijana wenyeji wawili ambao hapo awali walijajiriwa kama wasaidizi wa utafiti kwa kazi ya tathmini ya uvuvi kwa mwaka 2002 katika MUMARU: Bi. Saida Mwaimu na Bw. Kasimu Kindinda.
5. Msaidizi katika ndege, pengine mwindaji wa jadi: hakupatikana lakini baadhi ya wazee waliokaribishwa walikuwa wenye maarifa mengi kuhusu ndege.

Mkutano wa kwanza na kamati ya mipango na wasaidizi ulifanyika tarehe 22 Januari 2003.

Wasaidizi waliongelea kuhusu thamani ya mafuriko, wakieleza kuwa mafuriko yana faida nyingi kuliko hasara, na kwamba uzulishaji mali katika delta kunahusiana na mafuriko, kwamba mafuriko yanafanya matumizi ya mbolea ya viwandani kutokuwa muhimu Rufiji n.k.

Mahusiano ya utani na wakulima wa juu kutoka matumbi na milima ya kichi pia uliongelewa. Watu hawa daima chukuliwa na mafuriko lakini hawatambui ukuliwa wa uwanda wa mafuriko una faida ngapi. Mama Habibi Omari aliyafupisha yote vizuri kwa kusema kuwa anapendelea njaa inayoletwa na mafuriko mavuno ya kilimo cha mlao kuwa mazuri



na uvuvi huwa mzuri. Aliseama kuwa uwanda wa mafuriko wa Rufiji una misimu mingi ukilinganisha na kilimo cha nchi kavu cha mataifa.

Pia alisisitiza kuwa watu wa Rufiji wameyazoea mafuriko na lenye shughuli nyingi ambapo shughuli nyingi zinaweza kuunganishwa Mzee Masela alieleza upekee wa mikoko ya Rufiji na jinsi muingiliano kati ya maji ya chumvi na maji baridi unavyoweza kusababisha ulimbikaji wa udongo wenye rutuba sana. Alitilia mkazo kazi ya uchujaji maji ya ifanywayo na mikoko na faida ziletwazo na kitendo hiki kwa maji ya mwambao.

Alisisitiza kuwa kilimo cha mlao cha tegemezi ya chakula ni cha thamani na pia cha kutegemea zaidi kuliko aina nyingine za kilimo wilayani.

Wazee pia walikuwa na maarifa makubwa sana kuhusu ndege, wakibainisha aina mbalimbali za manufaa. Ndege wanaotangaza nvua, ndege wanaotangaza muda wa kupanda mazao, ndege wanaoonyesha maeneo mazuri kwa uvuvi, viongozi wa asali, ndege wanao toa tahadhari ya nyoka na wanyama wa hatari. Thamani za uzuri pia zilitajwa, kwa mfano uzuri za ndege. Ndege wengine (bundi) na sauti za ndege zinazoashiria kifo. Zilisimuliwa hadithi nyingi nzuri za ndege ambazo zingeweza kutumika wakati wa matembezi ya viumbe na pia katika kuandika rasimu ya yaliyomo katika picha kubwa ya ndege ya maonyesho (kiambatanisho cha 2). Mheshimiwa Palla alitoa msaada wa onyesho la kupendeza toka delta, kazi iliyokwisha /kubalika ya mfuniko ambao unafikiwa alifurika kiota cha ndege wa kichawi wa mnanzi.

Kwa kuna wafanyakazi wa elimu wa Wilaya walikuwa na majukumu mengine nyingi ya kushiriki kikamilifu, wawezeshaji wa nje wa programu ya elimu ya uzoefu ya mazingira (EUM), Kathryu Doody, aliobwa kushiriki katika maandalizi ya shughuli za kielimu, upangaji wa maonyesho, tathmini na uandikaji wa ripoti. Shughuli na maonyesho vilizingaioa program ya EEL, kijarida ambacho kiko katika matayarisho.

1.3 Kipindi cha mazoezi ya matembezi ya viumbe.

Mnamo tarehe 30, Januari, 2003, toka saa 12 mpaka saa 4 asubuhi kamati ya mipango na wasaidizi walipatikana walifanya mazoezi ya matembezi ya viumbe, kufahamu sehemu ambazo vikundi vingewimama na masuala ya kujadiliwa katika sehemu hizo. Wawekaji kumbukumbu za samaki na usawa wa maji kutoka utete na vijiji vya jirani pia walikaribishwa ili wachangie maarifa yao na kupeleka yale waliyojifunza katika maziwa yao.

Mwingiliano ulikuwa wa hiari na majadiliano ya wazi. Kwa ujumla wazee wangeweza kuchagua maeneo ambapo vikundi vingejifunza kitu fulani.

Kisha wakatoa maarifa ya asili kuhusu matumizi na thamani ya rasilimali maalum. Mara nyingi wafanyakazi wataalamu wangeweza kuongeza maelezo ya kisayansi ya uvumbuzi fulani na kutoa mifano toka maeneo mengine juu ya kile kinachoweza kuwa matokea ya usimamizi mbaya. Walieleza kuwa baadhi ya udongo kuzunguka ziwa unaweza kutambuliwa kwa wote wa majani mafupi. Baadhi ya udongo wa chumvichumvi hauna uoto kabisa na mitaro ya ajabu ya mmomonyoko inapita. Hili na hifadhi ya udongo na athari yake kwa Rufiji chini. Kawaida pamoja na uongezekaji wa ukataji miti yaliyochongoka na ya uharibifu zaidi na masuala mengine ya matumizi ya ardhi katika bonde yalionyeshwa. Nyavu za kuvulia majaribio lilifanyika a matunda madogo.

Udavi huu mdogo wa kupendeza na samaki wachanga walioachwa kutumika kuonyesha kazi ya kitalu cha kinamasi kawtika kingo za ziwa. Mtangi madogo ya maji alitumika kuonyesha mitego kwa washiriki lakini ingewezekana kuweka madumu rahisi ya jemu badala yake. Katika mbuyu kiota cha familia ya Hamerkop iligunduliwa. Wazee walieleza kuwa ndege huyu si moga kwa sababu haliwi. Kundi la korongo wenye midomo ya kuchongoka iliyo wazi ya kutafutia chakula waligunduliwa na kundi la viboko wanaokroma katika eneo



wanalotua samaki. Wazee walieleza kuwa nyama ya kiboko kimila hailiwi. Dhima ya viboko, kurutubisha maziwa kwa kinyesi chao ilijadiliwa. Kinyesi cha nguchiro kiligunduliwa. Jacana walionekana wakikimbia juu ya majani ya mayungiyungi maji na mfumo wao wa kupanda wa jike kupandwa na madume mengi (jike moja lina madume wengi wanaotunza mayai na vichanga ulifanya watu wakonyezane. Mdiria wa madoa doa walilazimika kuvnjaei karibu karibu. Baada ya kuriamasi, matembezi yalipita kwenye mashamba yenye rutuba ya uwanda wa mafuriko, kielelezo cha njia ambayo huweka vitu vidogo vidogo vyenye rutuba katika sehemu zenye kasi ya chini ya mkondo wa maji. Matembezi yaliishia katika muungano kati ya ziwa na mto ambapo A.S. Mwakalinga alieleza matumizi ya maandishi ya ubao wa jukwaani na dhima ya mafuriko kwa usambazaji maji kwenye maziwa.

Katika kipindi cha taarifa ya utekelezaji wakati wa staffahi iliyochelewa washiriki wote walithibitisha kuwa wamefurahia sana matembezi ya mazoezi na kuona mwungono wa maarifa ya kimila na yale ya kisanyansi yanaelimisha sana, kama ilivyokuwa ubadilishanaji wa uzoefu toka sehemu mbalimbali. Iliamuliwa kuwa vikundi viwili ni kima juu ambacho kingeweza kushughulikia wakati wa WWD halisi na kwamba vikundi vyote viwili vingefanya matembezi yaleyale lakini wakianza vituo tofauti. Wasaidizi waligawana katika vikundi. Wazee waliomba kuchukua nafasi kubwa katika maelezo yatakayotolewa kwa wageni waalikwa, walitilia maelezo yatakayotolewa kwa wageni waalikwa, walitilia mkazo kuwa ingekuwa bora kuendesha matembezi katika hali ya majadiliano ya wazi sawa na matembezi ya mazoezi kuliko katika muundo wa maelekezo toka juu kwenda chini. Iliamuliwa kuwa maonyesho hayana budi yakazie sana masuala yaliyoonekana katika matembezi ya viumbe kadri iwezekanavyo.

Kisha, kamati ya mipango iliandika rasimu ya ratiba ya mwisho kwa sherehe (kiambatanisho cha 3).

1.4 Kikundi cha Tathmini

Mkutano wa tathmini ulifanywa tarehe 3 February, 2003 wakati fikra za kumbukumbu bado tulikuwa nazo.

Kikundi cha tathmini kiliundwa na: Mheshimiwa Palla (mwenyekiti), Mheshimiwa Monero(Kamati ya Wilaya ya Huduma za Uchumi, Kazi na Mazingira), Mheshimiwa Mwajabu Kingwande, Bw. Peter John (katibu- DALDO), Bw. John Eniyoye (DGO), Bi. Saida Mwaimu, Bw. Kasimu Kindinda, Dk. Olivier Hamerlynck (CTA), Bw. Frederick Mhina (PM) Bw. Chande, Mzee Masela, Mzee Mnyige na Kathryn Doody.

Tathmini ilishughulikia kila moja ya mazoezi kwa zamu kwa kuuliza maswali yafuatayo:

- ✪ Ni lipi lilikuwa zuri na kwa nini?
- ★ Lipi halikuwa zuri na kwa nini?
- Ni kwa njia gani zoezi hili linaweza kuboreshwa?

Matokeo ya kina ya zoezi hili la tathmini yametolewa kwenye 2. Tathmini ya shughuli za sherehe (angalia chini).

1.5 Shughuli za baada ya tukio

Kwa kuchukulia kuwa tukio lilikuwa la mafanikio iliamuliwa kutayarisha haraka taarifa ya tovuti (kiambatisho cha 7) na kuipeleka kwa wote, Mkutano wa sekretarieti ya Ramsar na kwa IUCN. Taarifa hii ilikamilika tarehe 8 Februari. Ilitumwa kwenye tovuti zote mbili. Toleo la taarifa ya tovuti yenye rangi na tafsiri yake kwa Kiswahili, zilipelekwa kwa wageni wote waliokaribishwa kama ukumbusho wa tukio lililofanikiwa kwa wale walioshiriki na kama utani kwa wale ambao hawakushiriki. Ni matumaini kwamba watajutia kutohudhuria kwao na kwamba wataipa kipaumbele kwenye ajenda zao wakati ujao. Mwandishi aliyekuwepo wakati wa sherehe, Gratian Luhikula aliombwa kutayarisha toleo kwa ajili ya gazeti la taifa.



Majadiliano ya Matembezi ya viumbe kuhusu kazi za ardhi owevu katika Ziwa Lugongwe

2 Tathmini ya Shughuli za Sherehe

Sehemu hii itashughulikia kila moja ya shughuli kwa zamu, ikitoa maelezo mafupi na kisha kuifanyia tathmini shughuli yenyewe. Tathmini iko kwenye msingi wa majadilino ya kina ya kila shughuli iliyofanyika wakati wa mkutano wa tathmini, pamoja na taarifa ya nyongeza iliyotolewa na watu waliosimamia tukio hilo kwa siku hiyo.

2.1 Kupanga sherehe

Upangaji wa sherehe ulianza wiki 3 kabla ya tukio (angalia juu). Kamati ya mipango ilikutana mara kwa mara kupata taarifa ya maandalizi kutoka kwa wale waliosimamia vituo vya shughuli, kutathmini maendeleo na kupendekeza mibadala pale palipotokea kikwazo.

Tathmini

- ✪ Mchanganyiko wa maarifa ya kienyeji na maarifa ya kitaalamu ulikuwa ni mzuri kwa vile ulivyoleta masuala ya kitaalamu karibu na vile watu wa Rufifi walivyofikiri na kuhisi kuhusu eneo owevu na ndege.
- ✪ Upangaji ulitilia maanani thamani ya ujuzi wa asili.
- ✪ Uwekaji muda wa mipango ulikuwa mzuri, ulianza mapema, mikutano ya upangaji ilihudhuriwa vizuri (pamoja na zoezi la matembezi ya viumbe) na upangaji ulimalizika kwa wakati.
- ✪ Kuchanganya kujifunza kwa nadharia na kwa vitendo kulikuwa ni kuzuri kwa vile unaweza kuona hasa na kuelewa kile kilichotokea.
- ✪ Tafsihi nzuri baina ya Kiswahili na Kiingereza ilikuwepo wakati wa upangaji na hili lilikuwa muhimu.
- ✪ Ratiba iliyopangwa kwa siku hiyo inaonyeshwa kwenye ukurasa unaofuata.

- ★ Idara ya Elimu haikuwepo vya kutosha wakati wa upangaji kutokana na majukumu mengine. Labda kwa sababu hii, walimu wa shule hawakuhusishwa sana kwenye upangaji, licha ya ukweli kwamba mashule na wanafunzi ilikuwa ni hadhira lengwa muhimu na walihusishwa sana kwenye matukio. Kuwahusisha walimu katika hatua za upangaji kungewaruhusu walimu kuchangia kile wanachofikiria wanafunzi wanahitaji. Kwa kweli hatukutaka kuwashirikisha walimu katika hatua ya upangaji.
- ★ Sherehe zilifanyika mbali na mji/vijiji, katika siku zijazo sherehe hizi zinaweza kufanywa vijijini na mijini.
- ★ Mwakilishi wa kijiji cha majaribio hakuleta vifaa vya maonyesho hivyo hakuweza kuonyesha mafanikio yao katika usimamizi wa mazingira, na hata kuuza mazao yao yaliyotokana na shughuli za matumizi ya busara. Hii kwa kiasi fulani ilitokana na utata wa mawasiliano kwani waliambiwa kuwasilisha vifaa vya maonyesho kabla ya tarehe 30 Januari. Hili halikuwezekana kwa wawakilishi wa vijiji, kwani hiyo ingekuwa na maana ya kutumia siku 3 za ziada Utete, lakini kwa kweli wangeweza kuleta kwa urahisi vifaa vya maonyesho siku moja kabla ya tukio. Kwa nyongeza, uchaguzi wa mtu wa kuhudhuria tukio kama hili huchukua muda, ingawaje barua zilipelekwa siku 10/wiki kabla, kutokana na urefu wa muda unaohitajika ili barua kufika na hatua za uchaguzi, hakukuwa na muda wa kutosha kwa wawakilishi wa vijiji kutayarisha vifaa vya maonyesho. Kwa siku za baadaye barua za mialiko lazima zipelekwe mapema (zifike kijijini takriban wiki mbili kabla ya tukio), na inaweza kupendekezwa kwa vijiji vya majaribio watayarisha maonyesho bora mapema kwa ajili ya matukio kama hayo.

2.2 Kuzitangaza sherehe

Ilipangwa kuwa sherehe zingetangazwa kwa kutumia mabango ambayo yangewekwa katika sehemu muhimu. Kiasi cha watu wachache walisoma mabango, wapiga ngoma wenyeji wangekwenda nyumba hadi nyumba toka kwenye barabara ya kupitia ndege mpaka Bomani na kupita katikati ya Utete, wakipiga ngoma na kuwaambia watu kuhusu sherehe ambazo zingefanyika siku iliyofuata. Kwa nyongeza bendi ya shule iliombwa kutembea mjini ikipiga vyombo vyake wakati ikienda kwenye sherehe. Pia ilipangwa kuwa sherehe zingerekodwa na kutangazwa redioni.

Mabango mazuri yalitengenezwa na kuwekwa katika sehemu muhimu lakini hakukuwa na matangazo kwa ngoma kuzunguka mji na kutangaza habari hizo jioni ya tarehe 1 Februari.

- ✪ Mabango yalikuwa mazuri na yaliwekwa sehemu nzuri.
- ✪ Bendi ya ngoma ya wanafunzi iliyopita mjini na kuja mahali pa kujenga Mazingira mchana wa tarehe 2 ilikuwa njia ya kupendeza ya kuwahimiza watu kwenda kwenye sherehe – MMW aliuliza kama tunaweza kuangalia njia ambayo bendi hii inaweza kusaidiwa ili baadaye bendi ya pale kijijini, ya wanafunzi iweze kutumika kwa kutangazia na kukaribisha wageni kuliko kulipa pesa nyingi kwa bendi toka Dar es Salaam.
- ★ Mabango yalipangwa kuwa Utete mjini tu, wakisahau vijiji vya karibu.
- ★ Bwana Ndumbogani hakupatikana kurekodi na kutangaza matukio ya sherehe redioni kama ilivyopangwa.
- ★ Kiasi cha watu wazima wachache walikuja kwenye sherehe, labda kwa sababu mahali (watu wazima siku zote hawapendelei mikutano ya umma kwani wamechoshwa na ‘matukio ya kisiasa’ yenye hotuba ndefu sana, jambo ambalo tuliliepuka). Mara nyingine, kazi zaidi inahitajika ili kuboresha tatizo hili la mtazamo, labda kwa kufanyia katika eneo ‘lisilopendelea upande wowote’. Lakini moja ya madhumuni ilikuwa pia kuwafahamisha wakazi wa Utete kituo cha rasiimali katika misingi ya mazingira. Pia wakati mwingine wanafunzi wahimizwe kuja na wazazi wao kwenye matukio kama haya.
- Kwa siku za baadaye njia ya kupanga sherehe za kuonyesha Siku ya Ardhi owevu, Duniani na siku ya mazingira Duniani zichanganywe katika shughuli za shule.

2.3 Matembezi ya Viumbe

Matembezi ya viumbe yalipangwa asubuhi mapema ili kuonyesha wageni ndege na makazi kando ya ziwa Lugongwe. Matembezi ya zoezi yalifanywa ili kuanzisha njia na kuamua mada za majadiliano. Wazee walihusishwa zaidi katika shughuli hii, wakitoa na kuwasilisha taarifa nyingi zaidi. Bwana Mwakalinga alitoa mawasilisho akieleza njia za ukusanyaji wa data za maji na matumizi ya majukwaa ya maonyesho.

- ✪ Matembezi ya viumbe yalifanikiwa sana na tunatumia kwa ufanisi nyenzo na vifaa vyote (nyavu za kuvulia samaki zenye matundu madogo, matangi madogo ya samaki) kama ilivyopangwa.
- ✪ Matembezi ya viumbe yalifanya washiriki kutumia hisia zao zote.
- ✪ Mafanikio katika ufundishaji kuhusu dawa za asili.
- ✪ Mafanikio katika kuonyesha wazo la kuangalia viumbe kwa kujifurahisha na kuwa hiyo pia ni thamani ya ardhi owevu.
- ★ Wanafunzi kwa bahati mbaya wote walikuwa katika kundi moja, hivyo makundi ya umri hayakuchanganyika sana katika makundi haya mawili – hii ilikuwa kwa sababu

watu waliokuwa wakieleza wageni walichelewa kufika katika sehemu zao (na kwa sababu wanafunzi walikuwa wakiwakwepa walimu yalifanya wote waishie kwenye kundi moja.

- ★ Wanafunzi walichelewa kufika (kwa kweli hawakukaribishwa, lakini waliamua kuja wenyewe baada ya mazoezi ya kwaya ambayo kwa hakika ni dalili nzuri ya mapenzi yao) na hivyo walikosa maelezo toka kwa Mwakalinga kuhusu umuhimu wa kuweka kumbukumbu za data za usawa wa maji na viungo kati ya mto na ziwa.
- ★ Uwezo – kundi linalofaa, la watu 20 lilizidi kwa kiasi kikubwa. Katika kila kikundi kulikuwa na watu zaidi ya 40 hivyo vikundi vilikuwa vikubwa mno kwa mtindo wa majadiliano ya wazi ya masuala yatakayofanyika kwa njia ambayo ilifanyika wakati wa matembezi ya zoezi. Kwa kweli hii ina maana tunahitaji watu zaidi wenye uwezo wa kuongoza matembezi kama haya.



Kassimu Kindinda na washiriki wakiwasikiliza wazee na kujadili usimamizi wa uvuvi katika ziwa Lugongwe.

- Matembezi ya viumbe yalilenga ardhi owevu na ndege, hakukufanyika juhudi za kujadili masuala ya kawaida zaidi kama vile uchafuzi wa mazingira mf. kuwaomba washiriki wakusanye takataka. Kwa matukio ya baadaye masuala mapana zaidi yangeweza kujumuishwa.

2.4 Mchezo wa Kuvua Samaki

Mchezo wa kuvua samaki ni mchezo wa nje ambao huwahimiza washiriki watambue kuwa uvuvi usio endelevu huharibu akiba ya samaki na una athari mbaya kwa watumiaji wote wa rasilimali. Mchezo huu huhimiza washiriki kufikia mikakati ya usimamizi ili kuhakikisha maliasili za kawaida zinaendelea kutumika.

- ✦ Mchezo huu ulichezwa na vikundi kadhaa vya watoto waliojifunza kuhusu matatizo

yanayokabili usimamizi wa rasilimali za kawaida.

- ★ Mwezeshaji wa mchezo huu hakuwa na uhakika kama achezze mchezo huu na wanafunzi tu au pia na watoto wasiosoma shule. Kulikuwa na utata kutokana na idadi kubwa ya watoto waliokuwepo ambao shughuli zilikuwa kwa ajili yao. Wazo lilikuwa ilikuwa wazi kwa WOTE, hata hivyo ukweli ni kwamba kulikuwa na watoto wengi mno kwa wasaidizi kuwashughulikia.
- ★ Kutokana na ukosefu wa wasaidizi wa kuendesha mchezo kulikuwa na watoto wengi waliobaki wakisubiri bila kufanya kitu wakati wanafunzi walifurahia maonyesho ndani-mwishoni mchezo wa kuvua samaki ulichezwa na mtu yeyote.
- ★ Ilipendekezwa kuwa sherehe za baadaye walimu zaidi waandikishwe kusaidia kuwasimamia watoto kwani wamezoea kushughulikia makundi makubwa ya watoto.

2.5 Jedwali la Ugunduzi



Zoezi la jedwali la ugunduzi lilibuniwa ili kuwahimiza washiriki kuviangalia kwa makini vitu toka mazingira ya asili ambayo si ya kawaida, mazuri au yanafurahisha kuyaangalia. Ni bora vitu vilivyotumika vingekuwa vya kufurahisha kuvigusa, kuvipapasa au kuvinusa. Zoezi hili linawahimiza washiriki watumie hisia zao wanapochunguza kitu katika jedwali. Sehemu ya mchezo ilikuwa tu kulinganisha vitu katika jedwali na picha za kule vilikotoka, mf. mbegu za Mninga zinalingana na picha ya Mti wa Mninga, na kupata vile vilivyosalia ambavyo havikuwa na picha.

- ★ Zoezi lifanikiwa kwani washiriki wengi walivigusa, na kuvipapasa wakiviangalia kwa karibu vitu vilivyokuwa mezani. Tulifanikiwa kupata washiriki kutumia hisi zao nyingi 'kugundua' kitu.
- ★ Mwelekeo wa mchezo wa zoezi kulinganisha vitu na picha na kupata 'vilivyosalia nje' haukufanikiwa sana kwani washiriki walitatizika. Hii huenda tena ilitokana na idadi ndogo ya wasaidizi waliopatikana. Saida ambaye aliendesha zoezi hili alishawishika kusaidia kabla tu ya washiriki kufika na hivyo hakuwa na uhakika kabisa wa vitu vyote.
- Kwa siku za baadaye ingekuwa bora kulirahisisha zoezi hili kwa kuwauliza washiriki wanafikiri vile vitu ni nini na vinatoka wapi.
- Wahimiza walimu kuwa na jedwali la ugunduzi darasani ambalo mwanafunzi anaweza kuongezea vitu kwa ajili ya wanafunzi wengine darasani kuangalia, kugusa na kupapasa, wanafunzi wengine wanaweza kujaribu na kutafuta kitu hicho kinatoka wapi.



2.6 Mashindano ya uchoraji



Wiki moja kabla ya Siku ya Ardhi owevu Duniani shule za msingi za Siasa na Mapinduzi ziliombwa kushiriki katika mashindano ya uchoraji. Michoro iliwasilishwa kwa wakati muafaka (ilipofika Januari 30) kwa uamuzi. Dk. Olivier Hamerlynck na Kathryn Doody walizikagua picha na washindi watano walichaguliwa (mwamuzi wa tatu toka Idara ya Wanyama Pori ya Wilaya hakuweza kuhudhuria kwa sababu ya majukumu mengine). Michoro iliyoshinda ilionyeshwa katika mkutano wakati wa sherehe lakini nani alipata zawadi ya kwanza, ya pili n.k. ilifanywa siri mpaka wakati wa utoaji zawadi.

- ✪ Kulikuwa na picha nzuri nyingi zikionyesha ndege katika mazingira yao ya asili, nyingine zilikuwa na taarifa kuhusu ikolojia ya ndege, zikionyesha kuwa wanafunzi kweli walijua kuhusu ndege waliokuwa wakiwachora.
- ★ Michoro mingine ilichorwa katika karatasi hafifu sana na kufanya iwe vigumu kwa watoto kuchora vizuri.
- ★ Michoro haikutaja umri wa msanii. Kwa hiyo ilikuwa vigumu kutolea uamuzi wa haki – hasa kwa sababu ya kuwa wa kiwango cha umri wa watoto wanaosoma katika shule za msingi (wanafunzi wengine wa shule za msingi wako katika umri wa ujana). Matokeo ya mwisho yalikuwa kwamba washindi 3 kati ya 5 walikuwa wakubwa kuliko kwa kawaida inavyotegemewa kwa umri wa shule ya msingi (miaka 6 – 13).




- Kwa siku za baadaye inapendekezwa kuwa karatasi na vifaa vya kuchorea vitolewe kwa mashule ili wapewe wanafunzi kuchorea.
- Kwa baadaye inapendekezwa kuwa umri wa mchoraji uandikwe katika mchoro, ili michoro iweze kuamuliwa katika makundi mbali mbali ya umri.
- Ingekuwa vizuri picha ionyeshwe pamoja na msanii wakati wa sherehe ya kutoa zawadi.
- Pia, ili kuhakikisha kuwa anayeingia katika mashindano ni mchoraji kweli wa

picha hiyo, inashauriwa kuwa picha zichorewe shuleni.

2.7 Bango la ndege wa ardhi owevu

Hili lilikuwa bango lililotoa taarifa kuhusu aina za ndege wanaopatikana Rufiji. Kwa kuongezea taarifa kuhusu ikolojia ya ndege, wanaohama, jina la kisayansi, jina la Kiingereza na jina la kienyeji kulikuwa na maelezo mazuri sana yaliyoonyesha ndege katika mazingira yao ya asili. Chaguo la ndege walioonyeshwa lilifanywa kwa kuzingatia ndege wakuu wa ardhi owevu walioonyeshwa kwa kamati ya mipango na wazee na wanyama ambao huipa wilaya ya Rufiji umuhimu wa kimataifa. Nyenzo za nyongeza, tukirejea kwa ndege wa ajabu na wa kichawi, muhimu katika imani za kienyeji, zilitolewa na Mheshimiwa Diwani Pala.



- ★ Watu wengi walisoma bango hilo na walionekana wakijadili taarifa hiyo, hasa maafisa wa wilaya.
- ★ Majina ya kienyeji na Kiswahili hayakupatikana kwa aina zote za ndege.
- Ilipendekezwa kuwa muhtasari mfupi kwa watu kuchukua na kusoma ungekuwa wa manufaa.
- Kwa nyongeza kulielezwa haja ya kijitabu kidogo cha kupendeza kuhusu ndege wa Rufiji, hadhira lengwa ikiwa wafanyakazi wa wilaya na umma kwa ujumla.

2.8 Kona ya kupaka rangi



Kona ya kupaka rangi iliwapa watoto wadogo fursa ya kukaa na kupaka picha rangi au kufanya michoro ya nukta hadi nukta. Penseli, karatasi na picha za kupaka rangi zilitolewa.

- ★ Watoto wengi walifurahia upakaji rangi na kutoa kazi ya makini na kupendeza.
- ★ Ilikuwa vigumu kuwamudu watoto wote, kwani walikuwa wengi, picha ziliisha haraka
- ★ Kwa kuwa kulikuwa na watoto wengi, iliamuliwa kwa kusudi maalum kuwa

watoto wa shule tu wangepata nafasi ya kupaka rangi. Ilikuwa bahati mbaya kuwa watoto walioachwa (ambao hawakupata nafasi ya kwenda shule) walitengwa zaidi katika sherehe yetu.

2.9 Monyesho ya picha

Maonyesho ya picha yalionyesha picha za ndege wa misituni wanaopatikana katika Wilaya ya Rufiji

- ✪ Watu wengi walisimama kuangalia picha hizo na kuwajadili ndege waliowajua.
- ✪ Maonyesho yalivutia kuangalia na yalivuta uzingativu wa watu.
- ★ Kwa bahati mbaya hakukuwa na maandishi yaliyoeleza ndege wa msituni, wala madhumuni ya utafiti wa MUMARU wa ndege wa msituni wala maelezo kuhusu thamani ya aina mbali mbali za viumbe zisizo za kawaida zilizogunduliwa katika utafiti. Kwa hiy watu wengine hawakutambua ukweli kwamba picha hizo zilikuwa za ndege wa msituni, sio ndege wa ardhi owevu. Kutokuwepo kwa mtaalamu wa MUMARU aliyepata mafunzo ya ndege toka Idara ya Wanyama pori ya wilaya, aliyekuwa katika majukumu mengine (akishughulikia suala muhimu sana la simba katika uwanda wa mafuriko wa Kusini) ilikuwa sababu kuu ya ukosefu wa taarifa.
- Kwa baadaye hakikisha kuwa picha zina maandishi yanayotoa maelezo mafupi ya kile kinachonyeshwa na kwa nini tafiti hizi, zinazolenga wanyama wa viashiria, zinatoa orodha pana ya viumbe hai anuwai.

2.10 Gandisha maziwa katika mchezo wa ramani

Katika mchezo huu washiriki walitakiwa kugandisha maziwa ya karatasi gumu (kadibodi) yaliyokatwa katika ramani ya Mto Rufiji toka Mloka mpaka baharini, ukihimiza washiriki kufikiri kuhusu ni maziwa mangapi yaliyo Rufiji, yako sehemu gani, ni makubwa kiasi gani, nk. Ramani ilichorwa kwa kipimio cha 1:50,000 na si zaidi ya urefu wa m. 3.



- ✪ Mchezo huu ulichezwa na vikundi kadhaa vya wallimu na wanafunzi, wote wakiwa wameikamilisha ramani vizuri na walifurahia kucheza mchezo huu.
- ✪ Kikundi cha walimu kiliomba kuazima ramani hiyo wakaitumie shuleni kucheza zoezi hili hili na wanafunzi wao.
- ★ Kwa kuwa ramani ilionyesha Mto Rufiji na miji na vijiji vichache tu ilikuwa vigumu kwa washiriki kuelewa mazingira ya maziwa kuhusiana na alama nyingine za marejeo kama vile barabara na vijiji.



- ★ Baadhi ya washiriki hawakuutambua mto huo kuwa ni Rufiji - kitu ambacho kinaleta maana kama hujawahi kuona ramani ya Mto Rufiji na huna uzoefu ya kutumia ramani kwa ujumla.
- Kwa siku za baadaye ongeza sura zaidi katika ramani kama vile misitu, barabara, mikoko na vijiji – hili lingeweza kuwa zoezi la kufanywa na mashule.
- Ufuatiliaji wa ombi toka kwa walimu kutumia ramani hiyo shuleni.

2.11 Mchezo wa Mzunguko wa Maji

Mchezo huu ulikuwa na bango lililoonyesha mbetuo wa ubavuni mwa kilima, na miti, ziwa likiwa chini, mto, mawingu ya mvua na jua. Kusudi la mchezo lilikuwa kugandisha mishale ikionyesha yanakokwenda maji katika mzunguko wa maji, kisha kama washiriki waliweza waliambiwa kugandisha kitambulisho kuonyesha majina ya njia hizi mf. mvua, mvukizo, n.k.



- ✦ Wanafunzi wengi waliujaribu mchezo huu na kuufurahia wakijaribu kuweka mishale sehemu sahihi.
- ✦ Wanafunzi wengine, ambao hawakuliweza zoezi kikamilifu, walisaidiwa na Mwakalinga, ambaye alieleza kwa makini kanuni ya mzunguko wa maji. Mafunzo mengi yalifanyika?
- ★ Mchezo huu ulikuwa mgumu sana, hasa kwa wanafunzi wadogo.
- Kwa siku za baadaye mchezo huu ungeweza labda kurahisishwa kwa wachezaji wadogo kwa kuanza na taarifa zaidi ambazo ziko tayari katika bango.
- Labda zoezi hili linafaa zaidi kwa shule za sekondari.

2.12 Chemsha Bongo – Kutafuta maneno

Fumbo la kutafuta maneno (mifano imetolewa katika kiambatisho cha 4) lilibuniwa kwa ajili ya watoto wakubwa kufanya mazoezi ya stadi za maandishi kwa kutumia maneno ya mazingira.



sherehe hizi. Hasa kwa kuwa kulikuwa na kama nakala 40 hivi za fumbo zilizosalia ilipofika mwisho wa siku.

- ✦ Wanafunzi wengi walifurahia kucheza mafumbo haya na wakafanikiwa kukamilisha utafutaji maneno.
- ★ Kwa kuwa kulikuwa na watoto wengi iliamuliwa kwa makusudi maalum kuwa watoto wa shule tu wangepata nafasi ya kufumbua mafumbo haya. Ilikukwa bahati mbaya kuwa watoto waliokuwa wamekwisha achwa (ambao hawakupata nafasi ya kwenda shule) walitengwa zaidi katika
- ★ Mchezo huu uliishia kuamuliwa, ambalo haikuwa hasa dhana, ilikusudiwa kuwapa wanafunzi fursa ya kufurahia kufumbua fumbo na kufanya vizuri kadri walivyoweza.

2.13 Bango la Mimi ni Nani

Bango hili lilikuwa mchezo ambao washiriki walipaswa kubuni nini kilifichwa chini ya kifuniko, chini ya bango toka vidokezo 9 vilivyoonyeshwa katika mfuatano. Kama mshiriki aliweza kubuni picha ile ilikuwa nini bila kuiangalia picha hiyo walikuwa wameshinda. Vidokezo vilivyotolewa kwa kila picha vimeorodheshwa katika kiambatisho cha 5.



- ✪ Washiriki walielewa kwa urahisi jinsi ya kucheza mchezo huu na wengi walifanikiwa kubuni picha iliyofichwa.
- ✪ Washiriki walifurahia kucheza mchezo huu na kufanya mazoezi ya stadi za uainishaji.
- ★ Kwa kuwa kulikuwa na watoto wengi kulikuwa na umati mkubwa kuzunguka bango hivyo ilikuwa vigumu kwa watu waliokuwa nyuma kuona kilichokuwa kikitokea.
- Kwa siku za baadaye unda maswali/picha zaidi za kuchezea mchezo huu.

2.14 Mchezo wa Mimi ni Nani

Katika mchezo huu (uliochezwa nje) washiriki wanatakiwa kubuni kuna nini katika picha iliyofungiwa mgongoni kwake kwa kuuliza maswali 10, ambayo hadhira inaweza kujibu ndio au hapana. Huu ni mchezo wa kufurahisha ambao washiriki wanapaswa kufikiri kimantiki na kufanya mazoezi ya stadi za uainishaji. Inaonekana rahisi lakini ni ngumu vya kushangaza unapokuwa ndiwe mtu wa kubuni.

- ✪ Wanafunzi wengi walifurahia kucheza mchezo huu nje na mwalimu Mtwewe.
- ✪ Mchezo huu ni mzuri kwa kuwafanya washiriki wafikiri kuhusu jinsi mimea na wanyama na sura nyingine za mazingira zinavyopangwa katika makundi.
- ★ Mara nyingine tena watoto walikuwa wengi na hakukuwa na wasaidizi wa kutosha kuwasimamia – zoezi hili lingeweza kucheza katika makundi kadhaa madogo zaidi ikiwapa washiriki wengi zaidi nafasi ya kucheza kama kungekuwa na wasaidizi zaidi.
- Zoezi hili linaweza kutumika tena katika hali nyingi za aina mbalimbali kwani ni rahisi lakini linawafanya washiriki kufikiri kuhusu dunia ya asili inayowazunguka.

2.15 Mchezo wa Utando wa Maisha wa Ardhi owevu

Zoezi hili ni mchezo (ulichezwa nje) ambao washiriki wanapewa kadi ndogo inayoonyesha sura moja ya mazingira ya ardhi owevu, kama maji, miti, jua, nyasi, chura, samaki, ndege, mbu, mtu, n.k. Washiriki hukaa au kusimama kwenye duara na kurushiana mpira wa kamba unaowakilisha muungano kati ya kila moja wa washiriki (anayekula nini, anayehitaji nini kutengenezea kiota, n.k.). Hatimaye utando unaundwa. Endapo viungo/vitu vyote vya mazingira vinafanya kazi, utando unakuwa na nguvu na imara, hili linaweza kuthibitishwa kwa kuwaamuru washiriki waukandamize utando chini taratibu. Kiungo kimoja cha utando kisha huondolewa, ikielezea sababu zake, kwa mfano tukio la uchafuzi wa hali ya hewa linaweza likaharibu ubora wa maji ikiwa na maana ya kuwa wadudu na samaki wote watakufa, au bwawa lililoko upande wa juu wa

mtu litapunguza wingi wa mtiririko wa maji yake. Washiriki wengine itabidi waachie kamba pale vitu wanavyotegemea vinapokufa. Hatimaye utando wa maisha huanguka chini. Huu ni mchezo mzuri sana kwa kuonyesha uhusiano wa viumbe vyote katika mazingira.



- Zoezi hili linaweza kutumiwa tena katika hali tofauti kwani ni rahisi na huwafanya washiriki kufikiria kuhusu uhusiano kati ya viumbe hai katika ulimwengu unaowazunguka.

2.16 Mchezo wa Kuigiza

Kikundi cha Maigizo cha Utete kilikaribishwa kufanya mchezo mfupi wa kuigiza kuhusu umuhimu wa ardhi owevu na ndege. Kikundi hicho cha maigizo pia kiliombwa kutangaza sherehe zitakazofanyika Utete kwa kutumia ngoma, siku moja kabla ya tukio. Kwa bahati mbaya walikuwa na kazi nyingi bado za kuuboresha mchezo na hivyo kushindwa kwenda kutangaza tukio.

- ✦ Igizo lilikuwa zuri, lililoigizwa vizuri na kufurahiwa na hadhira.
- ✦ Igizo lilitumia vichekesho vema kuonyesha athari ya kuharibu makazi ya viumbe kwa jamii za vijijini na kusisitiza juu ya umuhimu wa ardhi owevu katika kudumisha maisha na kazi za mfumo wa ikolojia.
- ✦ Maigizo ni njia nzuri ya kufikisha ujumbe kwa hadhira.
- ✦ Igizo lililoonyeshwa na kikundi hicho lilibuniwa kwa kutumia nyenzo chache za nje – ikiashiria kuwa jamii ya wenyeji inaelewa umuhimu wa ardhi owevu.
- ★ Ujumbe wa kihifadhi mazingira unaotegemea jamii haukusisitizwa kwenye igizo.
- ★ Wazo la kutafuta ufumbuzi wa matatizo haukutiliwa mkazo katika mchezo huu wa kuigiza, badala yake wahalifu walishikwa na kuadhibiwa.
- ★ Katika igizo hili mtaalamu aliyekuja alitoka Japan – kwa nini isiwe Ulaya ili kuwa

karibu zaidi na ukweli?

- ★ Kikundi cha maigizo hakikusaidia kutangaza tukio siku moja kabla pale mjini.
- ★ Eneo la kufanyia maigizo halikuwa kubwa vya kutosha kwa kuwawezesha waigizaji kusambaa eneo lote.
- Kwa siku za baadaye fuatilia kikundi cha maigizo kwa karibu ili kuhakikisha maombi ya nyongeza kama vile kutoa matangazo kunafanyika au gawa kazi, ukiwapa watu wengine kazi ya kulitangaza tukio.
- Muhtasari wa kila onyesho uwe umeandikwa na kuwekwa kwenye kumbukumbu (katika Kiingereza na Kiswahili).
- Kwa matukio ya siku zijazo, andaa eneo la maigizo ama kwa kulaza kamba juu ya ardhi au kuweka jukwaa.

2.17 Kwaya

Shule za msingi za Siasa na Mapinduzi ziliombwa kutayarisha nyimbo za mazingira kuhusu ardhi owevu na kuziimba kwenye sherehe ya ardhi owevu duniani. Shule zilipewa muhtasari wa shughuli za ardhi owevu.

- ✳ Nyimbo za kwaya zilikuwa nzuri sana, za kuvutia, zikionyesha mambo ya siku yenyewe.
- ✳ Maneno ya nyimbo yalikuwa mazuri (hasa ya Shule ya Msingi ya Siasa) ambayo yalitoa mvuto wa hisia kwa watoa maamuzi kwa kuhakikishia kazi za ardhi owevu hata kwa vizazi vijavyo.
- ✳ Mahadhi na sauti zilijulikana kwa watu hivyo waliweza kukumbuka vipande vya nyimbo baadaye.
- ★ Eneo la kuimbia halikuwa kubwa vya kutosha kwa ajili ya waimbaji kuweza kujitandaza.
- Yachapishe maneno ya nyimbo na kutafsiriwa pia kwa Kiingereza, mpe Gratian Lukikula ili aweze kuingiza kwenye makala yake kwenye gazeti la taifa.
- Katika matukio ya siku zifuatazo liandae eneo la kuimbia, ama kwa kutumia kamba juu ya ardhi au jukwaa lililo inuliwa.
- Kwa siku zijazo eneo kubwa la kivuli linahitajika



2.18 Utoaji Zawadi



Ilipangwa kuwa wakati wa utoaji zawadi zingetolewa zawadi kadha wa kadha: Lars Dinesen angekabidhi kitabu cha IBA kwa Mkuu wa Wilaya; Washindi wa mashindano ya Uchoraji kupewa zawadi zao; makundi ya Kwaya kila moja kupewa Sh.T. 15,000/=; Kikundi cha Maigizo kupewa Sh.T. 15,000/=. Mashule kupewa zawadi zenye picha kubwa za ndege na taarifa za ardhi owevu.

- ✳ Muda wa kuanza kutoa zawadi ilibidi usogezwe mbele ili kumuwezesha Lars

kuwasilisha kitabu cha IBA kwa Mkuu wa Wilaya kabla ya Lars na wenzake kurudi Dar es Salaam. Hili lilikuwa jambo zuri na lililostahili kufanya ratiba irekebishwe. Lars aliwasilisha kitabu na kusema maneno machache akitilia mkazo thamani ya kipekee ya mazingira katika Wilaya ya Rufiji.

- ★ Mkuu wa Wilaya alimshukuru Lars lakini hakupewa nafasi rasmi ya kuongea – labda haikuwa lazima.

2.19 Uwasilishaji Wa Baiskeli Kwa Wakusanyaji Wa Data Za Maji

Ilipangwa kuwa wakusanyaji wa kujitolea wa data za usawa wa maji katika vijiji 6 watatia saina mikataba ya mapema siku ile na kupewa baiskeli zao.

- ★ Baiskeli zilitolewa baada ya maelezo mafupi ya kazi ya wawekaji kumbukumbu za usawa wa maji, na jinsi baiskeli hizo zitakavyotumika. Hadhira ilionekana kuelewa sababu ya kutoa baiskeli.
- ★ Baiskeli tatu tu zilitolewa hadharani badala ya 6 kama ilivyopangwa, hii ilikuwa ni kwa kuwa wapokeaji waliokusudiwa hawakuwepo.

2.20 Chemsha Bongo.

Ilipangwa kuwa chemsha bongo ya maswali 10 ingefanywa, watoto wakiulizwa maswali kuhusu umuhimu wa ardhi owevu na kuhusu ndege katika Rufiji. Maswali yameorodheshwa katika Kiambatisho cha 6.

- ★ Uamuzi wa kuchagua wawakilishi toka kila shule ulichukuliwa baadaye mchana lakini ulifanya kazi vizuri kuhimiza shindano.
- ★ Zoezi hili lilifanyika vizuri kama kichocheo kwa hadhira.
- ★ Njia nzuri ya kutolea maarifa.

- Kwa siku za baadaye itakuwa vizuri kama hadhira ingeziona zawadi, kwa kuwa zilikuwa zimefungwa katika bahasha hakuna aliyejua mwanafunzi alipata zawadi gani.
- Wazo hili la chemsha bongo lingehimizwa katika vyama vya mazingira vya mashule, pamoja na safari za ugani kwenda Selous na kwenye delta.



- Mkazo zaidi unahitajika kuvikuza na kuviendeleza vyama vya mazingira mashuleni, hii itahitaji msukumo toka kamati za mazingira za Wilaya. Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ameahidi kushughulikia hili pamoja na Idara ya Elimu.
- Hatua ya mpango wa mazingira ni muhimu zaidi kuliko matokeo (MUM). Ni muhimu kuwa na jumuiya ubaoni ili MUM itakayoandaliwa iweze kutekelezwa. Matukio ya kukuza mwamko na maudhui ya kitaalamu yanayohusiana ni njia nzuri ya kufanya hili.

2.21 Video

Ilipangwa kuonyesha video za mazingira/ardhi owevu jioni.

- ✪ Licha ya siku ndefu na iliyokuwa na shughuli nyingi, mahudhurio kwenye video yalikuwa mazuri na ilianza kwa wakati uliopangwa.
- ✪ Kulikuwa na makundi mbalimbali katika hadhira ya video, ikiwa ni pamoja na watoto, wanawake, wanaume na madiwani.
- ✪ Video nyingi zilizoonyeshwa zilikuwa kwa Kiswahili. Ie ya ardhi owevu za Uganda tu, iliyokuwa kwa Kiingereza ilitafsiriwa na Mwakalinga na kufupishwa mwishoni. Huu ulikuwa msaada mkubwa kwa kuboresha uelewa.
- ✪ Video ya ardhi owevu za Uganda ilikuwa nzuri katika kuzitia moyo biashara za uvuvi na ilionyesha kuwa hifadhi haikuwekewa mipaka katika Rufiji.

2.22 Mahudhurio

Orodha ya washiriki walioalikwa rasmi katika sherehe hizi iko katika Kiambatisho cha 8.

- ✪ Inakadiriwa kuwa watu 450 walihudhuria, wengi wao (takriban 300 wakiwa watoto).
- ✪ Mahudhurio ya umma kwa ujumla yalikuwa nzuri sana, kupita matarajio yetu.
- ★ Sherehe hizi zilihudhuriwa zaidi na wanawake kuliko wanaume, isipokuwa wageni toka vijiji vya majaribio ambapo uwiano wa kijinsia ulifikiwa.
- ★ Chama cha Kuhifadhi Wanyamapori cha Tanzania kilialikwa lakini hawakuweza kuhudhuria na waliomba radhi (WCST waliitwa kusaidia katika matembezi ya ndege). Mradi wa usimamizi wa mikoko pia waliomba radhi kwa kushindwa kuhudhuria kwa sababu ya majukumu mengine.
- ★ Kulikuwa na mahudhurio hafifu au hayakuwepo kabisa toka idara za wilaya zisizoshiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa shughuli za MUMARU ingawa masuala ya mazingira ni muhimu kwao, k.m. maendeleo ya wafanyakazi, maji, afya, kazi za umma na fedha.
- ★ Wengi wa wageni walikuwa watoto, inaelekea kuwa ujumbe haukuwafikia watu wazima wa Utete kwa njia iliyowafanya kuja na kuungana katika sherehe. Hii inaweza kuwa ilitokana na mahali pa sherehe, nje ya mji na karibu na makao makuu ya Wilaya huenda ili wafanya watu waamini kuwa lilikuwa tukio la kisiasa.
- ★ Kwa bahati mbaya kulikuwa na uhaba wa wafanyakazi wa Wilaya waliojitolea kusaidia shughuli hizi. Hii ilikuwa na maana kuwa wafanyakazi waliokuwepo, walikuwa na shughuli nyingi na walijitahidi kuimudu (bila kutegemea) idadi kubwa ya washiriki.
- Kutopenda tukio hili kwa idara nyingine itaorodheshwa katika TUM inayofuata. Njia za kuongeza ushiriki na uelewa wao zitatafutwa.

2.23 Mpango wa Jumla wa Sherehe

Siku nzima ilienda vizuri sana na karibu yote yaliyopangwa yalifanyika kwa mafanikio.

- Kwa siku za baadaye inapendekezwa kuwe na eneo kubwa zaidi la kivuli kwa ajili ya watu.

2.24 Tathmini ya Washiriki

Wakati wa kuondoka washiriki watu wazima wote walikaribishwa kujibu maswali yafuatayo kwa kuweka alama ya pato mhimili wa ndio au hapana:

1. Ulizifurahia sherehe?
2. Umejifunza kitu chochote?

Majibu ya washiriki kwa maswali haya yalikuwa kama ifuatavyo:

1. Ulizifurahia sherehe?

NDIO	31	(82%)
HAPANA	7	(18%)

Sababu kuu iliyotajwa na watu ambao hawakufurahia sherehe ilikuwa kwamba hawakupewa kinywaji cha bure (kwa sababu za bajeti hii ilikuwa kwa wageni waalikwa). Kwa siku za baadaye kiwango hiki cha maradufu kingerekebisha au kutolewa mibadala, kwa mfano kwa kukaribisha sekta binafsi kupanga jukwaa la kuuzia soda.

2. Ulizifurahia sherehe?

NDIYO	34	(85%)
HAPANA	6	(15%)

Ingeonekana kuwa idadi kubwa ya watu wazima hivyo wote walifurahia sherehe na kujifunza vitu. Tathmini zaidi ingefanywa kwa kupeleka hoja hizi mashuleni na pia TUM.

2.25 Mada nyingine Zilizoibuka wakati wa Majadiliano

Maonyesho – itakuwaje kwa maonyesho? Kamati ya tathmini iliamua hii ingekuwa bora iamuliwe na TUM.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Wilaya alitilia mkazo ukweli kwamba kwa miaka miwili iliyopita MUMARU ilionekana kutoka ofisini kwenda kwa watu. Hii ilifanya mradi uhusiane zaidi na Wilaya na jamii. Kwa kuwa na mashaka hapo mwanzoni kuhusu manufaa ya mradi sasa anaridhika kuwa awamu ya pili ni muhimu na inakaribishwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya tathmini alifunga mkutano kwa kumshukuru kila mmoja kwa ushirikiano wake, na kuhitimisha kuwa tulifanikiwa kwa 85%, hivyo bado kuna nafasi ya kuboresha zaidi kwa wakati ujao. Shukurani maalum zilitolewa kwa Dk. Olivier Hamerlynck na wazee kwa kujitolea muda na juhudi zao kwa sherehe hizi.



Ukumbi wa maonyesho kwanza ulifurika kwa washiriki waliokuwa na shauku, ni makundi ya watoto tu yaliyoruhusiwa kwa kufululiza kuingia kuchunguza na kujiunga katika michezo.

3 Viambatisho

3.1 Kiambatisho cha 1: Taarifa

Taarifa toka: Olivier Hamerlynck

Tarehe: 16 Desemba, 2002

Kwa: TACD, MM, TUM

Somo: Aina za Ndege Maji Kimataifa na Siku ya Ardhi owevu Duniani.

Aina za Ndegemaji Kimataifa ilianzishwa na Shirika la Utafiti wa Ndegemaji la Kimataifa (ambalo sasa limekuwa Ardhi owevu Kimataifa) miaka 25 iliyopita. Katikati ya mwezi Januari ya kila mwaka maelfu ya watu wa kujitolea hutoka kwenda kuhesabu ndegemaji duniani kote na data hukusanywa nchini na kuchapwa kama ripoti. Hii kisha hutumika katika kuchambua mwelekeo katika idadi ya aina fulani, nk. Katika nchi nyingi hili limekuwa zoezi la kufaa sana la kuinua mwamko kwa hifadhi ya ardhi owevu.

Kwa bahati mbaya Tanzania, kinyume na nchi nyingine nyingi za Afrika, zina wataalamu wa ndege wanaofanya kazi au wa ridhaa wachache sana na ukusanyaji wa data umekuwa mdogo kwa idadi ya korongo iliyochukuliwa angani katika maziwa ya Bonde la Ufa, mara nyingi na Wakenya. Itaonekana kuwa baadhi ya wafanyakazi wa Wilaya sasa wana maarifa ya kutosha ya ndegemaji kuweza kuchangia katika idadi ya kila mwaka na, kwa sababu mara nyingi tunasafiri katika maeneo ya ardhi owevu inawezekana kuhesabu, angalau baadhi ya aina za ndege maji maarufu (mwari, mnanzi, mbizi, bata na bata bukini, korongo, sipusipu, korongo domokijiko, kwara, tai samaki, mwewe weusi, viparara, nk). Inawezekana hata kuhesabu baadhi ya vitwitwi wakubwa (pamoja na kitwitwi wa taji jeupe Ndoero misuli, mwenye kelele wenye miguu ya njano na kijani na walio na upanga maarufu na sehemu kubwa nyeupe kwenye mbawa ambao katika Tanzania wanajulikana kutoka Rufiji tu). Je, baadhi ya wajumbe wa TUM na wake au waume wa wanakijiji watapendezwa kujitolea kwa hesabu ya ndegemaji yenye utaratibu katika safari zao ugani mwezi Januari? Ikiwa ndivyo tunaweza kuwa na kikundi kidogo kikipanga na kuratibu hesabu. Inabidi ieleweke vizuri kuwa hili si zoezi la malipo (posho). Kwa kujisikia kuwa sehemu ya mtandao wa mazingira ulimwenguni (fikiria ni watu wangapi wanaofanya kama hivi wakati unapohesabu, toka Alaska na Siberia mpaka Afrika ya Kusini na Terre del Fuego) na kuchangia ujuzi wa idadi ya ndege maji na usambazaji unaweza kupata hisia nzuri. Ingeweza kuchangia kwa maisha ya wenyeji kwa njia isiyo dhahiri kwa kuvuta usikivu wa wataalamu wa ndege na watu wengine wanaopenda mazingira kwa Rufiji. Hawa kisha wanaweza kuja na kutembelea na kutumia fedha kijijini kwa waongozaji, malazi, chakula, n.k.

Siku ya Jumapili, tarehe 2 Feburuari Dunia inaadhimisha siku ya Ardhi owevu Duniani. Tunaweza kuwa na mawazo kuhusu jinsi ambavyo tungependa kusherehekea siku hii katika Rufiji? Wazo moja ambalo tayari limeshatolewa ni kwa kuutumia ujuzi tulioupata katika zoezi la Elimu ya Uzoefu kuwapeleka watoto katika utafiti wa viumbe hai anwai wanaopatikana kwa urahisi katika ardhi owevu. Lakini tafadhali acheni akili zenu zitafute kwa uhuru mapendekezo mengine.

3.2 Kiambatisho cha 2: Maandishi ya Kiswahili na Kiingereza ya



A: SOCIO-ECONOMIC VALUES

1. Provide habitats for several species of birds, reptiles, fish, hippos etc.
2. Microclimate stabilization: rainfall and temperatures.
3. Food production: rice, pumpkins, sugarcane and maize.
4. Food provider: fish, prawns, and hippos.
5. Site for recreation and social functions: swimming, birdwatching, nature photography, sacrifices, sailing and sport-hunting.
6. Source of building and handicraft materials: palm, mangrove poles and pots.
7. Medicines for human and animals.
8. Water transport: canoes, boats and ships.
9. Water for domestic use: cooking, washing and bathing.
10. Drinking water and pastures for livestock and wild animals.
11. Breeding sites for some animals and birds.
12. Source of salt

B: ECOLOGICAL FUNCTIONS

1. Water balance: charging and discharging of lakes and underground aquifers.
2. Shoreline stabilization and erosion control.
3. Sediment and nutrient retention: sinks for Nitrogen and Phosphorus from agriculture and industries and by so doing improves the water quality and prevents eutrophication.
4. Nutrient transport: flood-fed agriculture cropping season in the Rufiji Floodplain.
5. Transport of various plant seeds and hence facilitate their distribution downstream.
6. Flood control: due to wetland's water storage capacity and ability to release runoff evenly.
7. Support mangrove forests and other forest resources.



MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA WILAYA YA RUFJI (MUMARU)

A. MANUFAA YATOKANAYO NA ARDHI OEUVU/ CHEPECHEPE

1. Makazi kwa viumbe kama vile ndege, mamba (na jamii zingine za mijusi), samaki, kiboko n.k.
2. Husaidia kurekebisha hali ya hewa, hasa mvua na kiwango cha joto
3. Kuzalisha chakula:- Mpunga, Maboga, Miwa na mahindi
4. Kuzalisha chakula:- Samaki, Kamba, Kiboko
5. Sehemu za kuburudika, kupunga upepo, shughuli za kijamii na kiutamaduni:- kuogelea, kuangalia ndege, kupiga picha, matambiko, matembezi ya boti na uwindaji mahalia.
6. Chanzo cha vifaa vya Ujenzi na zana za mikono:- Ukindu, nguzo za Mikoko na vyungu
7. Madawa ya binadamu na wanyama, hutoa kuni kwa ajili ya matumizi ya binadamu, Usafiri wa majini, Mitumbwi, boti na meli.
8. Maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani:- kupikia, kuoshea / kufua, kunywa na kuogea
10. Maji ya kunywa na malisho kwa mifugo na wanyama pori
11. Maeneo ya kuzaliana kwa baadhi ya wanyama na ndege
12. Hutoa chumvi kwa matumizi mbalimbali

B. MANUFAA YA KIIKOLOJIA

1. Husaidia kurekebisha uwepo wa maji ardhi kwa kuongeza na kupunguza maji ya maziwa na ya ardhi.
2. Kuimarisha kingo za ufukweni na kuzuia mmomonyoko wa udongo.
3. Husaidia kutuwamisha virutubisho hasa vya nitrojeni na phosphorus kutoka katika kilimo, viwanda na kwa kufanya hivyo huboresha ubora wa maji.
4. Kusafirisha virutubisho kwa ajili ya Kilimo cha mlao.
5. Husafirisha mbegu za miti, mazao na samaki mbalimbali
6. Kurekebisha mafuriko kwa kuruhusu maji kupita kwa uwiano mzuri.
7. Husaidia kuboresha misitu ya mikoko na rasilimali nyingine za misitu.

3.3 Kiambatisho cha 3: Bango La Ndege

Bango hili lilionyesha michoro mikubwa, picha ndogo za ndege, ramani za njia za kuhama nk. Orodha kamili ya ndege waliogunduliwa Rufiji na kipande cha mfuniko wa kiota cha mnanzi wa kichawi vilionyesha kama viambatisho katika bango.

BAADHI YA AINA YA NDEGE WENYE SIFA KUBWA WILAYANI RUFJI

Wilaya ya Rufiji inaweza kufananishwa na Peponi katika suala la ndege. Wilaya ina aina zaidi ya 420 za ndege kati ya aina 1100 za ndege zinazofahamika na kuwekwa katika orodha Tanzania. Aidha bado aina nyingi za ndege zinasubiri kutambuliwa hapa. Tanzania kwani bado kuna ndege zaidi ya 120 ambao hujumuishwa/hushirikishwa katika kundi hili la ndege wa maeneo chepechepe hawajaorodheshwa.

Tanzania imegawanywa katika kanda za mraba zipatazo 350, na aina zote za ndege waliopo katika kila eneo hutambuliwa na kuwekwa katika orodha maalumu ya ndege. Wilaya ya Rufiji kwa mtizamo huu ina maeneo 4 ya mraba kati ya 350 ya Tanzania (angalia ramani).

Katika maeneo bora 80 ya ndege yaliyoandikwa Tanzania, maeneo 3 yapo wilayani Rufiji kama ifuatavyo:

- Eneo la hifadhi ya wanyama Selous
- Misitu ya pwani ya wilaya ya Rufiji (Kati ya misitu hii ya pwani yetu, ni Misitu ya Matumbi, Vilima vya Kichi na Ngumburuni tu ambayo imeshafanyiwa uchambuzi wa kufahamu ndege waliyopo)
- Maeneo ya Visiwani (Delta)

BAADHI YA AINA YA NDEGE WILAYA YA RUFJI WANAONYESHA UASILI NA UMUHIMU WA RUFJI.

Jina la Kienyeji	Jina Kiingereza	Jina la Kisayansi
Mtepe	African Skimmer	<i>Rynchops flavirostris</i>

Ndege mwenye mabawa marefu, mwenye weusi na weupe anafahamika sana hapa Rufiji na huonekana hasa mwisho wa mafuriko. Wazee husema huashiria mwisho wa mafuriko, kwa hiyo ni mwanzo wa kilimo cha Mlau. Sehemu yake ya chini ya mdomo ambao una rangi ya chungwa iliyoiva ni mrefu kuliko sehemu ya juu ya mdomo. Hali hii inamwezesha kuishi vizuri katika maeneo chepechepe na kukamata samaki katika maeneo ya mito yenye tope. Ndege huyu huruka karibu sana na usawa wa maji, wakati mwingine pembeni mwa mto huku akikata maji kwa kutumia sehemu ya chini wakati mwingine pembeni mwa mot huku akukata maji kwa kutumia sehemu ya chini ya mdomo kama kisu. Kila samaki mdogo atakayepitiwa na sehemu hii ya mdomo hunaswa na kuchukuliwa/ kuliwa. Baada ya kula ndege huyu kuburudika ufukweni. Sehemu hizi pia huzitumia katika kutaga na kutamia mayai yake. Mafuriko yanapofika tena ndege huyu hutoweka katika maeneo haya; bado haijulikani anaelekea wapi, lakini inaaminika labda huelekea ziwa Nyanza/Victoria. Ndege hawa ni wachache sana katika Afrika. Huonekana hasa katika maeneo ya mito yenye mafuriko. Hata hivyo ndege huyu ameshatoweka katika maeneo mengi ya mito yaliyojengwa malambo/mabwawa.

Jina la Kienyeji	Jina la Kiingereza	Jina la Kisayansi
Sipu Sipu	Pied Kingfisher	<i>Ceryle rudis</i>

Kati ya aina 9 ya Sipu Sipu wanaofahamika hapa Rufiji huyu anayetajwa sasa anaonekana sana na

huonekana hasa katika sehemu zenye samaki wengi na uvuvi wa sehemu hiyo ni mzuri.

Ndege huyu huwinda kwa kutumia uwezo wake mkubwa wa kuona. Huruka juu ya maji huku akiangalia samaki, mara aonapo samaki, husimama angani/ sehemu alipo samaki na kumnyemelea hadi atakapomkamata. Kama atabahatika kumkamata samaki, basi huruka naye hadi ufukweni na kuanza kula. Mara nyingi akishakamata samaki huhakikisha kuwa amemua samaki kwa kugonga kichwa chake kwenye mti.

Huweka kiota chake katika mashimo yaliyopo katika kingo za mto.

Jina la Kienyeji	Jina Kiingereza	Jina la Kisayansi
Mchingu	Hamerkop	<i>Scopus umbretta</i>

Pengine huyu ndege ni kati ya ndege wa majini ambaye huweza kuonekana katika wilaya ya Rufiji kwa urahisi. Mara nyingi huja karibu na sehemu ya kuvulia smaki na kuchukua mabaki ya samaki yaliyoachwa. Anafahamika sana hasa pia kwa uwezo wake wa kutengeneza kiota kikubwa katika mti. Kiota hiki huonekana kama nyumba yenye mfuniko katika tawi la mti. Kiota hiki huweza kukaa kwa muda wa miaka mingi na pengine ndege wengine wadogo wakaanza kujenga na kuisha nje ya kiota hiki.

Jina la Kienyeji	Jina Kiingereza	Jina la Kisayansi
Kopwangola	African Open-billed stork	<i>Anastomus Lamelligerus</i>

Ndege hawa huonekana zaidi katika kingo za maziwa, maeneo owevu, na katika mashamba chepechepe. Mdomo ya ndege hawa imefanana na chombo cha kushikia kitu (bapa) ila ina mwanya katikati. Mdomo huu umeumbika hivyo ili uweze kukamata konokono kwa urahisi majini au katika matope. Ndege hawa hushirikiana sana, huonekana katika makundi, wakati mwingine kundi huwa na ndege 1000 waliokaa ufukweni. Wakati wa usiku ndege hawa hulala katika mti mkubwa kwa pamoja. Kama walivyo Mwewe na Tai, ndege hawa wana uwezo wa kutumia upepo wenye joto umbao unawasaidia kuruka bila kupeperusha mbawa. Hali hii inawasaidia waweze kusafiri umbali mrefu bila kuchoka.

NDEGE WA VISIWA VYA RUFUJI

Visiwa vya Rufiji vikiwa na misitu ya Mikoko yenye hektari 50,000 na maeneo wazi yanayoonekana wakati wa maji kupwa, ni maeneo muhimu sana kwa ndege wa maeneo chepechepe/owevu katika Afrika. Zaidi ya ndege hawa 40,000 walihesabiwa mwezi Desemba 2002. Hawa ndege badala ya kuishi/kula usiku au mchana kama ndege wengine, wameweza kuishi kufuatana na kukupwa kwa bahari. Hujilisha kwa masaa sita katika maeneo yenye tope na kichanga na wakati wa maji kujaa hukaa katika misitu ya mikoko kwa masaa sita. Baadhi ya aina za ndege wenye sifa za kimataifa waliopo katika visiwa vya Rufiji ni hawa wafuatao:-

Jina la Kienyeji	Jina Kiingereza	Jina la Kisayansi
Kitwitwi Domosululu	Curlew sandpiper	<i>Calidris ferruginea</i>

Ndege hawa wadogo huweka viota vyao katika vichaka vya asili huko Siberia karibu na Ncha ya Kaskazini ya dunia, sehemu ambayo huwa na barafu kwa muda wa miezi 9 ya mwaka. Katika mwezi Machi na Aprili ndege hawa huanza kujilisha kwa nguvu mno na kujiwekea mafuta mengi mwilini, kuongeza uzito karibu gramu 50 hadi 80. Kwa mfumo huu wa kula na kuhifadhi chakula, ndege hawa huweza kuruka umbali mrefu zaidi ya maelfu ya Kilomita hadi watakapofika katika maeneo mazuri kwa kula tena na kuzaana. Baada ya kuzaana hurudi tena kwa mfumo ule ule na kufika tena katika visiwa vya Rufiji mwezi Oktoba. Wanaweza pia kuruka hadi Afrika kusini. Ndege hawa wapatao 16,000 walihesabiwa katika visiwa mwezi Desemba 2000. Hii ni sawa na

zaidi ya asilimia 2 ya idadi ya ndege hawa duniani.

Jina la Kienyeji
Kitwitwi Kijivu

Jina Kiingereza
Terek sandpiper

Jina la Kisayansi
Xerus cinereus

Ndege huyu huzaliana katika maeneo ya Taiga, misitu ya misindano ya Siberia kusini mwa Tundra. Katika Rufiji, wanapenda kula katika maeneo ya mifereji yenye matope katikati ya misitu ya mikoko. Hudidimiza midomo yao katika matope haya na kutafuta minyoo ya ardhini. Ndege 2900 walihesabiwa katika visiwa mwaka 2000, karibu asilimia 6 ya idadi ya ndege hawa duniani. Ndege wengi hawakuweza kuhesabiwa kwani boti iliweza kupita katika mifereji mikubwa na yenye maji mengi tu.

Jina la Kienyeji
Ndoero

Jina Kiingereza
Crab Plover

Jina la Kisayansi
Dromas ardeola

Huwa ni ndege wanaoonekana sana na wana rangi nyeuse na nyeupe. Ndege hawa hula zaidi jamii ya kasa wadogo. Huzaliana zaidi katika visiwa katika bahari nyekundu na Huba ya Persian. Ndege wapatao 3500 walihesabiwa katika visiwa mwezi Desemba 2000, karibu 12% ya idadi yao duniani.

Jina la Kienyeji
Mnandi

Hakuna jina la kingereza na pia la kisayansi

Ndege huyu ni wa ajabu sana. Ndege huyu hufikiriwa ni wa mazingara. Hata hivyo hakuna mengi yanayoeleweka juu ya ndege huyu. Inafikirika kuwa ndege huyu si rahisi kuonekana kwani huishi chini ya bahari. Wakati mwingine mabaki ya kiota chake hutoka chini ya bahari na kutupwa na maji ufukweni. Mganga anasema kiota hiki hutumika katika uganga wa kumfanya mtu asionekane. Mambo mengine ya ndege huyu yanaonekana ni siri ya ndani lakini hata hivyo labda kuna ukweli ndani yake.

3.4 Kiambatisho cha 4: Ratiba

SHEREHE ZA SIKU YA ARDHI OWEVU DUNIANI

RATIBA YA MATUKIO

UTETE - TAREHE 2 FEBRUARI, 2003

MUDA	TENDO	MAHALI
12.00 – 4.00	Matembezi ya Viumbe Kukutana katika njia Panda ya Hospitali, kugawanyika katika makundi mawili	Ziwa Lugongwe na Darajani
4.00 – 8.00	Mapumziko	
8.00 – 9.00	Maonyesho na Michezo Sehemu ya I Kila mmoja anakaribishwa kuangalia maonyesho na kujiunga katika shughuli.	Kiwango cha Mazingira.
9.00 – 9.20	Kwaya ya Shule ya Msingi ya Siasa	Kiwanja cha Mazingira
9.20 – 9.40	Onyesha la Kikundi cha Maigizo cha Utete	Kiwanja cha Mazingira
9.40 – 10.00	Kwaya ya Shule ya Msingi ya Mapinduzi	Kiwanja cha Mazingira
10.00 – 10.30	Maonyesho na Michezo Sehemu ya II Kila mmoja anakaribishwa kuangalia maonyesho na kujiunga katika shughuli.	Kiwanja cha Mazingira
11.30 – 11.00	Chemsha bongo (John au Mhina)	Kiwanja cha Mazingira
11.00 – 11.10	Kutoa Baiskeli kwa wakusanyaji data za maji (Mwakalinga)	Kiwanja cha Mazingira
11.10 – 11.30	Kutoa zawadi Kutoa Kitabu Muhimu cha Eneo la Ndege kwa DC (Na Lars Dinesen au Mwakilishi) Zawadi za shindano la Uchoraji Kwaya Maigizo Shule	Kiwanja cha Mazingira
12.00 – 2.00	Onyesho la video Kila mmoja anakaribishwa kukaa na kuangalia video za mazingira	Chumba cha Mikutano.

3.5 Kiambatisho cha 5: Jedwali la maneno

Maneno nane yaliyojificha katika jedwali lifuatalo hapa chini.
 Unaweza kuyatafuta yote?
 Moja limefanywa (Panya) kukusaidia.
 Herufi lazima ifuate nyingine katika msari ulionyooka

P	A	N	Y	A	S	M
O	N	Y	O	K	A	T
P	M	A	U	A	X	U
O	T	N	D	E	G	E
W	S	I	M	B	A	H

Maneno yanaweza yakaenda kulia au chini, lakini sio nyuma

Panya Ndege

Maua Simba

Nyoka Nyani

Mtu Popo

Jedwali la maneno – Kiingereza

Maneno nane yaliyojificha katika jedwali lifuatalo hapa chini.
 Unaweza kuyatafuka yote?
 Herufi lazima ifuate nyingine katika mstari ulionyooka.
 Maneno yanaweza yakaenda kulia au chini, lakini sio nyuma.

Wetland
 Marsh
 Lake
 River
 Water
 Mangrove
 Hippo
 Crocodile
 Heron
 Kingfisher
 Fish
 Stork
 Snail
 Dragonfly
 Python
 Eel
 Crab

F	D	R	A	G	O	N	F	L	Y
I	Z	X	E	S	T	O	R	K	T
S	N	A	I	L	A	P	O	I	Y
U	A	S	D	H	E	R	O	N	I
F	G	H	J	K	C	L	Z	G	H
Q	M	W	E	C	R	A	B	F	I
M	A	N	G	R	O	V	E	I	P
Y	R	T	R	I	C	C	X	S	P
U	S	V	N	V	O	V	B	H	O
I	H	O	B	E	D	T	N	E	N
W	A	T	E	R	I	L	U	R	M
I	U	W	E	T	L	A	N	D	L
L	Y	A	L	E	E	K	U	J	O
P	Y	T	H	O	N	E	O	I	P

Jedwali la maneno

Maneno nane yaliyojificha katika jedwali lifuatalo hapa chini.

Unaweza kuyatafuta yote?

Herufi lazima ifuate nyingine katika mstari ulionyooka.

Maneno yanaweza yakaenda chini, lakini sio nyuma.

ARDHI OWEVU
CHEPECHEPE
ZIWA
MTO
MAJI
MIKOKO
KIBOKO
MAMBA
SIPUSIPU
SAMAKI
KERENG'ENDE
KONOKONO
NYOKA
KAA
MAWINGO
MAFURIKO
CHATU
CHURA

M	O	S	A	M	A	K	I	L	M	I
K	M	A	M	B	A	I	A	C	A	V
O	G	H	J	Q	X	B	X	H	J	S
N	Y	O	K	A	E	O	M	E	I	I
O	M	T	O	C	Z	K	A	P	R	P
K	A	R	D	H	I	O	W	E	V	U
O	J	G	F	A	W	H	I	C	C	S
N	I	U	R	T	A	W	N	H	H	I
O	K	Z	X	U	C	Y	G	E	U	P
M	A	F	U	R	I	K	O	P	R	U
K	A	A	Q	B	N	M	I	E	A	T
J	K	E	R	E	N	G	E	N	D	E
Q	E	U	Y	P	M	I	K	O	K	O

Jedwali la maneno – Kiingereza

Maneno nane yaliyojificha katika jedwali lifuatalo hapa chini.

Unaweza kuyatafuta yote?

Herufi lazima ifuate nyingine katika mstari ulionyoka.

Maneno yanaweza yakaenda kulia au chini, lakini sio nyuma.

Water Cycle Word Search
EVAPORATION
PRECIPITATION
RAIN
CLOUDS
SNOW
ICE
WATER
LIQUID
STEAM
VAPOUR
TRANSPIRATION
RUNOFF
EROSION
WET
DROUGHT
FLOOD
MIST

M	O	W	S	T	E	A	M	E	T	A	I	S	L
I	G	H	J	L	V	A	P	O	U	R	I	N	I
S	I	O	P	K	A	D	R	O	U	G	H	T	Q
T	R	A	N	S	P	I	R	A	T	I	O	N	U
U	A	T	C	L	O	U	D	S	R	E	W	Q	I
Y	I	C	E	J	R	H	G	N	F	D	S	A	D
W	N	J	K	L	A	E	R	O	S	I	O	N	X
E	V	B	N	M	T	Q	U	W	A	T	E	R	Z
T	P	R	E	C	I	P	I	T	A	T	I	O	N
C	V	R	U	N	O	F	F	K	W	A	C	K	L
K	N	M	L	K	N	F	L	O	O	D	E	G	A

3.6 Kiambatisho cha 6: Mimi ni nani? Unaweza kubuni kilichofichwa

chini ya kifuniko, chini? Mawazo ya maswali.

Chura

Mimi si mmea.
Sina manyoya wala magamba.
Nina miguu minne.
Daima ninaishi karibu na maji lakini mara nyingine utanikuta katika nchi kavu.
Ninahitaji hewa safi.
Ninataga mayai.

Ninaweza kuruka na kutambaa, na kuogelea vizuri sana.
Ninakula wadudu.
Simdhuru binadamu.

Mdudu alaye Popo

Mimi si mmea.
Ninaishi katika nchi kavu.
Nina manyoya na kuzaa watoto hai
Ninaishi katika majengo, miti na mapango.

Ninakula wadudu wengi, pamoja na mbu.
Kwa kawaida ninalala muda mwingi mchana na kuamka jua lituapo.
Ninatoa aina mbali mbali za sauti pamoja na mlio mkali na miluzi.
Ninawinda kwa kutumia sauti kuonyesha mawindo yangu.
Nina mabawa na ninaweza kurua kwa kasi sana.

Samaki

Mimi si mmea.
Siwezi kutembea, sina miguu.
Sina manyoya.
Ninaishi katika maji.

Ninaweza kupumua majini.
Ninakula vitu vingi, pamoja na wadudu na majani.

Binadamu hupenda kunikamata na kunila.

Ninataga mayai.
Ninaweza kuogelea vizuri sana.

Mti

Mimi si mnyama.
Ninaishi katika nchi kavu.
Kwa kawaida nakua pole pole sana.
Ninaweza kukua kupita urefu wa m. 50.
Ninatoa mbegu na matunda yazae tena.
Ninatumia mwanga kukua

Ninapopumua ninatoa oksijeni katika angahewa

Ninaweza kuishi kwa mamia ya miaka.

Nina manufaa sana kwa binadamu.

Ziwa

Mimi si mnyama wala mmea.
Ninaweza kuwa mkubwa au mdogo.
Unaweza kujiona ndani yangu.
Mimi ni mzuri kwani ndani yangu unaweza kuona rangi katika mbingu na uakisi wa mazingira yangu.
Ninaweza kuwa mviringo au mrefu na mwembamba.
Ninakuwa mkubwa mvua inaponyesha.
Ninawapatia binadamu chakula na maji.
Ninaweza kuwa na kina kirefu au kifupi.
Nina vitu vingi vinavyoishi ndani yangu, pamoja na samaki, viboko na mamba.

3.7 Kiambatisho cha 7: Maswali na majibu ya Chemsha Bongo

(Kiswahili na Kiingereza)

1. ELEZA KIREFU CHA KIFUPISHO MUMARU, PIA TOA SHUGHULI TATU ZINAZOFANYWA NA MUMARU

JIBU: Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji; Utafiti, shughuli endelevu za maendeleo ya Maliasili (Ufugaji wa nyuki, Kilimo hai cha matunda, Kilimo mseto), kutoa ufahamu na elimu ya kusimamia maliasili.

2. ELEZA UMUHIMU WA MAENEO CHEPECHEPE HASA KWA MAISHA YA WATU WA RUFJI

JIBU: Maeneo chepechepe yanadumisha maisha ya wananchi wa Utete kwa kutoa chakula kupitia kilimo, uvuvi, wanyama pori. Aidha maeneo haya hustawisha aina mbali mbali za maliasili ambazo ni vyanzo muhimu vya uchumi wa wananchi.

3. TAJA JINA LA UJUMLA/KUU LINALOWAKILISHA MISITU YOTE INAYOSTAWI KATIKA MAJI CHUMVI, KANDOKANDO YA VISIWA, MITO NA BAHARI YA HINDI

JIBU: Mikoko

4. TAJA AINA 4 ZA SAMAKI ZINAZOPATIKANA KATIKA MABWAWA, MITO NA VISIWA KATIKA WILAYA YA RUFJI

JIBU: Perege, kumba, pele, kambale, vitoga n.k

5. TAJA AINA 3 ZA NDEGE WANAOPATIKANA KATIKA MAENEO CHEPECHEPE YA WILAYA YA RUFJI

JIBU: Bata maji, Sipu sipu, Mchingu, Kopwangola n.k

6. TOA SABABU 3 ZA KUONYESHA KWA NINI NDEGE NI MUHIMU KWA JAMII YETU YA RUFJI NA TAIFA KWA UJUMLA

JIBU:

Husaidia kusambaza mbegu za mimea

Wanakula wadudu waharibufu wa mimea

Wanakula nyoka ambao wangukuwa ni tishio la maisha ya binadamu na wanyama wengine endapo wangukuwa wengi (Husawazisha idadi ya nyoka)

Ndege ni wazuri na ni kivutio

Wanatuburudisha kwa sauti zao nzuri

Baadhi yao ni chakula

Chanzo cha fedha za kigeni

7. TAJA JINA MOJA LA NDEGE ANAYEWEZA KUOGEELEA KATIKA MAJI, PIA ELEZA KWA VIPI MAUMBILE YAKE YALIVYOUMBIKA ILI KUMWEZESHA KUOGEELEA

JIBU: Bata maji, kwasababu miguu yake iko kama utando wa buibui pia nyoya zake zinatelezesha maji.

8. TAJA AINA YA NDEGE WA PORINI AMBAYE WANANCHI WA RUFJI SASA WAMEANZA KUMFUGA

JIBU: Kanga

9. TAJA FAIDA 3 ZA ZILETWAZO NA MAFURIKO YA MTO RUFJI

JIBU: Mazalio ya samaki huongezeka, maji ardhini huongezeka, Hurutubisha udongo, husaidia katika kurekebisha mzunguko wa maji, chanzo cha maji ya binadamu na wanyama wengine, hujaza maziwa/mabwawa na pia ni sehemu ya mazalio ya ndege na wanyama wengine wa majini.

10. TOA SAUTI YA NDEGE YEYOTE WA PORINI; KISHA KWA SIRI MNONG'ONEZE MSIMAMIZI WA KIPINDI HIKI JINA LA NDEGE HUYO

(JIBU: Atalitoa anayetoa sauti)

Maswali na Majibu ya Chemsha Bongo (Kiingereza)

1. What is REMP? Give examples of what REMP is doing.

Answer: Rufiji Environment Management Project, Activities – Research, Sustainable Development Activities (beekeeping, organic horticulture, agroforestry), Awareness and Education.

2. What is the Importance of Wetlands for the livelihoods of the Rufiji people.

Answer: Rufiji wetlands support life for the inhabitants and outside world by providing **FOOD** in terms of agriculture (crops), fisheries and wildlife; wetlands support and produce several kinds of **NATURAL RESOURCES** which are major sources of income for people.

3. Name the famous type of forest that grows in salt water along the coast of the Western Indian Ocean. (Needs good Kiswahili version).

Answer: Mangrove Forests

4. Name 4 types of fish found Rufiji Lakes and Delta.

Answer: Tilapia, Pele, Kambale, Vitoga etc.....

5. Name 3 types of waterfowl found in the Rufiji Wetlands.

Answer: Ducks, Geese, Snipe, Comorants, Storks, Egrets, King fishers etc.

6. Give 3 reasons why birds are important to the community and the Nation.

Possible Answers:

Seed Dispersal.

They feed on insects and mammals that can be crop pests, keeping the population in check.

They feed on snakes that could be harmful, keeping the population in check.

They are beautiful and decorate our lives.

They entertain us with their sounds/songs and displays.

Food - they are a source of protein (chickens, ducks, guinea fowl ostrich etc.)

Source of foreign exchange – bird watching, photography holidays for tourist.

7. Name a bird that can swim in water, and how is it adapted to water?

Answer: Duck, adaptations, webbed feet, waterproof oil feathers.

8. Name a type of wild bird that is commonly reared by people in Rufiji.

Answer: Guinea Fowl

9. Name 3 beneficial affects of floods.

Answer: Fish Production, Ground Water Re-charge, Natural Fertilisation of the floodplain, regulates water cycle, water supply for humans and animals, fills up the lakes, habitat for breeding birds.

10. Make the sound of a wild bird (tell the quizmaster which bird it is and if the audience can guess correctly what the bird is you get the prize)

3.8 Kiambatisho cha 8: Taarifa ya tovuti Utete Inasherehekea Siku ya Ardhi owevu Duniani

Hatimaye, baada ya wiki za matayarisho mapambazuko ya Siku ya Ardhi owevu Duniani yamefika. Kwa ahueni kubwa ya kamati ya mipango, usiku ulimalizika na kuanza kwa asubuhi iliyokuwa na mawingu kidogo lakini hakukuwa na mvua. Kuondoka nyumbani wakati wa giza kuliongeza shauku, kadri idadi ya watu ilivyokuwa ikiongezeka katika maandamano iliungana nasi kwenda kwenye fukwe za Ziwa Lugongwe karibu na Utete katika wilaya ya Rufiji, Tanzania. Maandamano haya marefu yalijumuisha wazee, viongozi wa kienyeji walioheshimiwa ambao maarifa yao ya jadi yalikuwa ni muhimu katika matayarisho, lakini pia walimu, wanafunzi, watoa maamuzi, wafanyakazi wa wilaya ya Rufiji na wageni waliokaribishwa kutoka mbali kama vile Denmark.



Pale ambapo pwangola, wakiwa kwenye viota vyao juu ya miti, walitua ukingoni mwa maji na kuanza kula, tulianza matembezi yetu ya kutembelea viumbe. Tukitembea kwenye maeneo chepechepe na ya matete tulisimama mara kwa mara ili kusikiliza mnana akiimba, au kuangalia kiboko akijitokeza juu ya maji na kurusha maji, au kujadili ni kiasi gani ardhi owevu ni muhimu kwa watu wa Rufiji. Mifano ni rahisi kuiona kuzunguka mto Lugongwe: Ugavi wa maji wa ji wa Utete yanavutwa kutoka mtoni, kuna ardhi yenye rutuba kwa kilimo, virutubisho vyake vikiongezwa kila mwaka kwa mafuriko na uvuvi hutupatia chakula na nafasi za biashara. Watafiti wawili vijana wa uvuvi waliwaeleza watembeaji jinsi usimamizi wa rasilimali za ziwa zinavyoweza kuboresha ubora na wingi wa samaki. Walionyesha mfano wa Mtanza Msona, kijiji cha jirani ambako wavuvi wenyeji wamefanikiwa kukubaliana kuhusu ngambi ya uvuvi wa samaki ziwani.



Bibi Habiba, mmoja wa wazee, alivuta usikivu wa vijana na sio watoto wakati alipoeleza matumizi ya dawa za asili za mimea ya ardhi owevu lililohusika. Wanafunzi walifurahia kutumia vionambali kuangalia ndege wa Sile wakitua taratibu juu ya majani ya mayungiyungi, au kuangalia sipu sipu wakitua, kwa utaratibu wakisubiri samaki chini ya maji. Lundo la magamba yaliyovunjwa vunjwa jirani ya mwamba lilichochea majadiliano moto moto kuhusu aina za wanyama ambao wangeweza mara kwa



maru kutumia mwamba kama fuawe. Muafaka wa mwisho (kukiwa na msaada mdogo kutoka kwa wazee wetu) ulikuwa: nguchiro wa ardhi chepechepe akipondapona konokono kupata nyama. Tulipofika darajani upande wa pili wa mlizamu kati ya



Ziwa na Mto mkubwa wa Rufiji tulimkuta Mwakalinga (Afisa kilimo wa wilaya) aliyeonyesha jinsi ya kupima usawa wa maji katika ziwa na kueleza umuhimu wa ukusanyaji wa data za usawa wa maji ili kujaribu na kuelewa hatua za ikolojia katika kazi Rufiji, lakini pia kugundua mielekeo ya muda mrefu. Data hizi zinatumiwa kurekebisha mtiririko wa maji katika Rufiji. Viashiria vya kwanza ni maziwa, muhimu sana kwa maisha ya watu na kwa wanyama pori wa ndani, yatakauka au kuwa chumvi chumvi bila ujazwaji tena wa kila mwaka kwa mafuriko. Ukweli kwamba mafuriko haya yanazidi kutishiwa na maendeleo ya unakoanzia mto, haukuepuka mtazamo wa umma na maswali mengi yaliulizwa.

Hali ilipoanza kuwa joto sana katika eneo la wazi tulikimbilia kivulini, bado tukijadili masuala yaliyoibuka wakati wa matembezi.

Saa 8 mchana Bendi ya Matarumbeta ya Shule ya Msingi ya Siasa kwa shauku ilitangaza mwanzo wa shughuli za mchana, wakiimba na kucheza kupitia mjini na kuleta mamia ya watoto wengine kwenye viwanja vya mazingira katika mdundo wake. Baada ya utangulizi mfupi na ukaribisho kwa sherehe, wageni walianza kuchanganyika na kutalii chumba cha maonyesho na maktaba, iliyojengwa na mradi wa usimamizi wa mazingira Rufiji (MUMARU). Kulikuwa na mazoezi mengi kwa makundi ya marika yote, watoto wadogo walipaka picha rangi, karibu kuwakaribia washindi wa shindano la uchoraji, ambao juhudi zao zilionyeshwa katika ubao wa mbali. Watoto wakubwa walifanya mchezo wa mzunguko wa maji na wakaonekana zaidi upenda mafumbo ya kutafuta maneno ya ardhi owevu.



Wengine walijaribu kubuni picha zilizofichwa toka dondoo zinazoeleza tabia ya wanyama na mimea.



Chumba cha maonyesho mara kilifurika watoto waliojaa shauku wakiropoka ropoka, wakisongamana kuzunguka mazoezi na mabango ya taarifa. Ilikuwa nafuu kujipenyeza mlangoni kwenda kuangalia shughuli za nje. Katika pembe mbali mbali za kiwanja wawezeshaji walikuwa wakicheza michezo ya mazingira na makundi makubwa ya watoto. Mchezo wa Mtandao wa Maisha wa Ardhi owevu ulionyesha mwingiliano wa mahusiano ya vitu vingi tuvionavyo kutuzunguka, wakati

mchezo wa uvuvi wa samaki ulikuwa ukiwahimiza watoto kuhusu athari za uvuvi uliokithiri na kubuni ufumbuzi wao wenyewe wa usimamizi.

Halimashauri ya Wilaya ya Rufiji inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji pamoja na msaada wa kitaalamu toka IUCN, Umoja wa Hifadhi Duniani na kufadhiliwa na Ubalozzi wa Ufalme wa Uholanzi, Dar es Salaam, Tanzania. Kwa taarifa zaidi wasiliana na iucndar@epiq.or.tz.


Sehemu ya kuvutia kwa siku hiyo ilikuwa inaonyesha Shule ya Msingi ya Mapinduzi na kwaya ya Shule ya Msingi ya Siasa. Maneno ya nyimbo, mahadhi na uchezaji ulikuwa wa ajabu, ulijaa uhai na kwaya ilitoa ujumbe mzito kwa wazazi, watoa maamuzi na wakazi wote wa Rufiji ukiwaomba kulinda maisha yao ya baadaye kwa kuhifadhi ardhi owevu.



Makundi ya watoto yalika chini na watu wazima kuangalia igizo fupi la Kikundi cha Maigizo cha Utete. Ilitumia vichekesho na futuhi kwa ufanisi kuchunguza athari za haribifu wa mazingira katika jamii za vijijini, na kusisitiza umuhimu wa ardhi owevu katika kudumisha kazi za mfumo wa ikolojia na maisha ya vijijini.




Lars Dinesen na Mzamilu kaita toka Makao Makuu ya Idara ya Wanyama pori Wizara ya Maliasili na Utalii walitoa kitabu kipya kabisa cha Important Bird Areas of Tanzania, (maeneo muhimu ya Ndege Tanzania) kwa Mkuu wa Wilaya ya Rufiji. Maeneo muhimu ya ndege matatu kati ya 80 yaliyoorodheshwa katika kitabu hicho yako katika wilaya ya Rufiji. Kisha Mkuu wa Wilaya ya Rufiji alijtoa zawadi kwa washindi waliofurahi wa shindano la uchoraji, ikifuatiwa na zawadi kwa kwaya, kikundi cha maigizo na shule za msingi.



Zoezi la mwisho la mchana lilikuwa Chemsha Bongo. Wanafunzi toka shule mbili za msingi walitakiwa kujibu maswali kuhusu ardhi owevu na Ndege wa Rufiji katika chemsha bongo.

Baada ya giza kuingia video za elimu ya mazingira zilionyeshwa na kujadiliwa na licha ya siku ndefu na iliyokuwa na mishughuliko mingi, ukumbi ulijaa.

Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa wilaya za Utete na Rufiji kuadhimisha Siku ya Ardhi Owevu Duniani. Kwa kweli imeinua mwamko na huwezi kujua, huenda kisiwa cha Rufiji, kilicho na eneo kubwa zaidi la mikoko katika Afrika Mashariki na makazi ya zaidi ya ndege maji 40,000 linaweza kuwa eneo la Ramsar hivi karibuni. Waandalizi waliochoka walifurahishwa na mafanikio ya tukio hili, na wako tayari kufanya mipango ya upeleka sherehe hizi katika ngazi ya kijiji mnamo mwaka 2004



3.9 Kiambatisho cha 9: Orodha ya washiriki walioalikwa katika sherehe za Siku ya Ardhi owevu Duniani

1	Mkuu wa wilaya
2	Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
3	Mwenyekiti (Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji)
4	Katibu wa Utawala wa Wilaya
5	Mwenyekiti (Kamati ya Mazingira)
6	WEO – Utete
7	Diwani (Utete)
8	Wakuu wa Idara (nje ya TUM)
	a) Maendeleo ya Wafanyakazi
	b) Idara ya Maji
	c) Afya
	d) Idara ya Kazi
	e) Idara ya Fedha
	f) TSC
	g) Kituo cha Ukoma Kindwitwi
9	Wajumbe wa TUM:
	a) Maliasili – Wakuu wa Idara
	b) Kilimo
	c) Maendeleo ya Jamii
	d) Ardhi
	e) Wanyama Pori
	f) Uvuvi
	g) Misitu
	h) Mipango
	i) MMP
	j) RUBADA
	k) TATEDO
	l) RUBEP
	m) Elimu
	n) Mheshimiwa Athuman Palla
	o) Mheshimiwa Mwajabu Kingwande
10	Waalikwa Maalum:
	a) Mwakilishi Idara ya Wanyama Pori
	b) Mwakilishi WCST
	c) Gratian (Luhikula, mwandishi)
11	Wasaidizi:
	a) Wazee – wawindaji/wavuvi – watu 6
	b) Wawekaji kumbukumbu za usawa wa maji toka maziwa ya jirani watu – 6
	c) Bi. Saidi Mwaimu
	d) Bw. Kasimu Kindida
	e) Bw. A. Mwakalinga
	f) Bw. Haji Mkungura
12	WANAVIJIJI
	a) Wanakijiji 2 – Mtanza/Msona
	b) Wanakijiji 2 – Mbunju/ Mvuleni
	c) Wanakijiji 2 – Jaja
	d) Wanakijiji 2 – Twasalie
	e) Wanakijiji 2 – Wanafunzi 25 (Shule ya Msingi ya Siasa)
13	Walimu na Wanafunzi
	a) Walimu 20 –Shule ya Msingi ya Mapinduzi
	b) Walimu 12 – Shule ya Msingi ya Siasa
	c) Wanafunzi 25 – Shule ya Msingi ya Mapinduzi
14	Kikundi cha Maigizo - watu 6